# UJAGINA WA MWANAMKE KATIKA *PANGO*

**NA**

**MUNIU GEORGE GITHUCI**

**C50/65581/2011**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI IDARA YA KISWAHILI**

**NOVEMBER 2013**

## IKIRARI

Tasnifu ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa katika chuo kingine chochote kile,kwa minajili ya kutosheleza shahada ya uzamili.

**MTAHINIWA**

**Sahihi _________________________ Tarehe ___________________**

**MUNIU GEORGE GITHUCI**

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu sisi tulioteuliwa na chuo kikuu kusimamia

**Sahihi _________________________ Tarehe ___________________**

**DKT AMIR SWALEH**

**Sahihi _________________________ Tarehe ___________________**

**DKT HEZRON MOGAMBI**

# TABARUKU

Naitaburuku kazi hii kwa wazazi wangu wapendwa marehemu Edward Muniu na Grace Njeri Muniu kwa kujitolea mhanga na kujifunga mkwiji barabara kama barabara za bara kunilea na kunielimisha. Aidha nawavulia kofia kwa kuniadilisha, maadili ambayo yamenipa msingi wa utubora nilionao. Mterehemezi awaweka mahali pema peponi hadi siku ya kiama inshalla tutakapokutana.

## SHUKRANI

Naam, ni dhahiri shahiri kuwa, kukamilika kwa tasnifu hii kumewahusisha waja wengi mno. Ni muhari kuwataja wote; hata hivyo nitakuwa mkavu wa fadhila andapo sitawataja wafuatao: Dkt. Amir Swaleh na Dkt. Hezron Mogambi kwa usaidizi,uongozi, mlahaka na ulelekezi katika mchakato mzima wa kuandika tasnifu hii. Waama, wamekuwa mithili ya mboni ya jicho langu. Maulana awajalie Sudi Saada sufufu.

Aidha shukrani za dhati ziwaendelea wahadhiri wengine wote wa idara ya Kiswahili Chuo Kikuu Cha Nairobi walionisomesha bila kuonyesha utepetevu wowote tangu nilipokuwa zumbukuku hadi sasa ninapojiona fahali mwenye fahari ya kumiliki shahada ya uzamili(masters). Hawa ni pamoja na Prof Kineene, Prof. Habwe, Prof. Mberia, Prof. Wamitila, Dtk. Iribe,Dkt Jefwa, Dkt. Zaja, Dkt. Timammy, Dkt. Mbatiah, Dkt. Mbuthia, Dkt. Musyoka, Dkt. Mukhwana na Bw. Mungania. Maulana awazuruku maradufu na ashei.

Nawashukuru vilevile mke wangu mpendwa nana Norah na watoto wangu akina Hilda, Jane, Maria na Hellen kwa uvumilivu na hamasa zao walizonipa hasa nilipokuwa karibu kukata tamaa kutokana na changamoto nyingi kwenye bahari ya usomi.

Shukrani za kidugu nawapokeza wasomi wenzangu wote tulioshirikia nao kama kiko na digali katika majaribio magumu na mazito ya kiusomi. Nyinyi nyote nitawakumbuka miaka na mikaka, enzi na dahari.

Shukrani za moyoni aidha ziwaendee walimu wote tunaofanya kazi nao wakiongozwa na kinara wetu Ustadhi Micheal Kihiu kwa uvumilivu wao na shime za kila wakati. Kongole na jalali awajalie neema kochokocho.

Shukrani zisizokifani pia ziwaendelea Bi. Eunice na Bw. Peter Rugu walioipiga chapa kazi yangu kwanzia mwanzo hadi mwisho. Kwenyu kutoke mema na kurudi mema.

Mwisho na washukru wasimamizi wote wa Chuo Kikuu Cha Nairobi kwa kutupa mazingara ya kiusomi. Endapo kuna mwengine yeyote ambaye si kutambua na amechangia kwa njia moja ama nyingine katika kufanikisha tasnifu hii, naomba msamaha.

# MUHTASARI

Tasnifu hii inahakiki ujagina wa mwanamke katika *Pango.* Mwongozo wetu katika kazi hii ni nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika. Inalenga kuibua ujagina wa mwanamke katika jamii inayoongozwa na mfumo kandamizi wa ki-ubabedume. Tumeigawa kazi hii katika sura tano. Sura ya kwanza imeshughulikia tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti, nadharia tete, sababu ya kuchagua mada ya utafiti, upeo na mipaka ya tasnifu, msingi wa nadharia, yalioandikwa kuhusu somo hili na hatimaye njia za utafiti. Sura ya pili imeshughulikia ujagina wa mwanamke na asasi za jamii. Asasi hizi tukasema ni pamoja na dini, ndoa na elimu. Sura ya tatu inahusu ujagina wa mwanamke unavyodhihirika katika *Pango*. Sura ya nne imeshughulikia wahusika wengine wanavyochangia ujagina wa mwanamke katika *Pango.* Hatimaye sura ya tano ni hitimisho ambapo muhtasari wa matoke ya utafiti, mapendekezo pamoja na tafiti za baadaye zimeshughulikiwa.

**YALIYOMO**

Ikirari.................................................................................................................ii

Tabaruku ..............................................................................................................iii

Shukrani ...............................................................................................................iv

Muhtasari ..............................................................................................................vi

Yaliyomo..............................................................................................................vii

**SURA YA KWANZA UJAGINA WA MWANAMKE KATIKA *PANGO* ................ 1**

1.0 Utangulizi ......................................................................................................... 1

1.1Tatizo la Utafiti ................................................................................................. 2

1.2 Madhumuni ya Utafiti ...................................................................................... 2

1.3 Nadharia Tete ................................................................................................... 2

1.4 Sababu za Kuchagua Mada Hii ........................................................................ 3

1.5 Upeo na Mipaka ya Tasnifu ............................................................................. 3

1.6 Msingi wa Nadharia ......................................................................................... 4

1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Somo Hili ................................................................. 14

1.8 Njia za Utafiti ................................................................................................ 17

**SURA YA PILI: UJAGINA WA MWANAMKE NA ASASI ZA JAMII ................ 18**

2.0 Utangulizi ....................................................................................................... 18

2.1 Dhana ya Ujagina ........................................................................................... 18

2.2 Aina za Ujagina .............................................................................................. 19

2.2.1 Jagina Chanya .............................................................................................. 19

2.2.2 Jagina Hasi/Danganyifu ............................................................................... 19

2.2.3 Jagina Pwaya/Kinzani .................................................................................. 19

2.3 Sifa za Ujagina. .......... 20

2.4 Asasi za Jamii .......... 21

2.4.1 Asasi ya Dini .......... 21

2.4.2 Asasi ya Ndoa .......... 24

2.4.3 Asasi za Elimu .......... 27

**SURA YA TATU: UJAGINA WA MWANAMKE UNAVYODHIHIRIKA KATIKA PANGO .......... 29**

3.0 Utangulizi .......... 29

3.1 Dhihirisho la Ujagina Wa Katango Miongoni Mwa Wazee .......... 30

3.1.1 Mchango wa Vijana Katika Kuudhihirisha Ujagina wa Katango .......... 38

3.2 Pingamizi Na Changamoto Zinazomkabili Katango Katika Kuudhihirisha Ujagina Wake .......... 41

3.2.1 Utangulizi .......... 41

3.2.2 Ngwese: Mwakilishi Wa Utamaduni Kandamizi .......... 42

3.2.3 Babake Katango: Ishara Ya Upinzani Dhidi Ya Ujagina wa Mwanamke. .......... 43

3.2.4 Mbabekazi kama Mwakilishi Wa Mfumo wa Ki-ubabedume .......... 45

3.3 Hitimisho .......... 46

**SURA YA NNE: WAHUSIKA WENGINE WANAVYOCHANGIA UJAGINA WA MWANAMKE KATIKA PANGO .......... 48**

4.0 Utangulizi .......... 48

4.1. Wahusika wa Kiume Wavyochangia Katika Kuudhihirisha Ujagina Wa Mwanamke Katika Pango. .......... 48

4.1.1 Kibwana Kama Mshiriki Katika Kuudhirisha Ujagina W$a Katango .......... 49

4.1.2 Kikubi: Ishara ya Kujitolea kwa Vijana Kuudhihirisha Ujagina wa Mwanamke. .. 52

4.1.3 Babu: Kiwakilishi cha Umoja Wa Kizazi Kipya na Kizazi Cha Kale..................... 54

4.1.4 Sota kama Mwakilishi wa Vijana Katika Kuunga Mkono Ujagina Wa Katango.... 56

4.1.5 Mama Katango: Ishara ya Ushirikiano wa Wanawake........................................... 57

4.1.6 Sakina: Ishara Ya Muungano wa Wanawake ......................................................... 60

4.1.7 Susa kama Ishara ya Mwamko Mpya wa Wanawake............................................. 61

4.2 Hitimisho................................................................................................................... 62

**SURA YA TANO: HITIMISHO ...................................................................... 64**

5.0 Utangulizi.................................................................................................................. 64

5.1 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti .............................................................................. 64

5.2 Mapendekezo ........................................................................................................... 66

5.3 Tafiti za Baadaye ...................................................................................................... 66

**MAREJELEO ............................................................................................................ 68**

# SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

Historia ya utanzu wa tamthilia katika fasihi ya Kiswahili ni changa ikilinganishwa na tanzu za Riwaya na Ushairi. Kwa ufupi, utanzu huu ulianza kujitokeza kati ya mwaka 1950 na 1957. Tamthilia zilizoandikwa wakati huo ni pamoja na *Afadhali Mchaw i*(1957), *Mgeni Karibu*(1957) za Graham Hyslop, *Nakupenda Lakini*(1957) ya Henry Kuria miongoni mwa nyingine. Maudhui mengi katika tamthilia za wakati huu hayakuwa yakikweza mila, desturi na tamaduni za kiafrika bali kuwatukuza wakoloni.

Baada ya uhuru, waandishi wa tamthilia ya Kiswahili kama: E. Hussein katika *Wakati Ukuta* (1971), P. Muhando katika *Hatia* (1974) walianza kushughulikia maudhui ya hali za maisha ya wakati huo. Maudhui haya yalihusu masuala ya ukombozi wa kisiasa na kuwajibika kwa viongozi. Tamthilia *Mashetani* (1971) ya E. Hussein inamulika masuala ya kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Tamthilia nyingine za wakati huo ambazo zilikuwa zinajadili masuala ya kijinsia ni pamoja na *Hatia* (1972), *Nguzo Mama* (1982), za Penina Muhando; *Mama ee* (1987) ya Ari Katini Mwachofi; *Heshima Yangu* (1974) na *Lina Ubani* (1984) za Penina Muhando. Kwa jumla, maudhui yaliyojitokeza katika tamthilia tulizozitaja awali ni pamoja na miito ya kutambuliwa kwa haki za wanawake, hasa nafasi ya mwanamke katika masuala ya kijamii, kiuchumi, na kisiasa. Mengine ni kuhusu jinsi asisi za kijamii kama ndoa, dini na utamaduni zinavyomnyima mwanamke nafasi katika mawanda mengi ya maisha na hivyo, kumsonga na kumnyonga katika maendeleo ya kijamii.

Asasi hizi zimemsukuma pembeni na kumfunga pingu mikononi na kumyima uhuru na uwezo wake kama mlezi wa jamii. Waama amenyimwa haki sawa na mwanamume

Hali ya kusikitisha ambayo tumeichambua hapo juu ndiyo iliyotuchochea kutafitia swala la ujagina wa mwanamke katika tamthilia ya *Pango*, ya K.W Wamitila.

## 1.1 TATIZO LA UTAFITI

Tatizo la utafiti huu, ni swala la ujagina wa mwanamke katika tamthilia ya *Pango* ya K.W. Wamitila. Aidha tutachambua kwa kina pingamizi anazopatana nazo mhusika mkuu katika kuudhihirisha ujagina wake. Mwisho tutawamlika baadhi ya wahusika wasaidizi wanaoukamilisha ujagina huu.

## 1.2 MADHUMUNI YA UTAFITI

i) Tunadhamiria kuchunguza ukweli na uhalisia unaozingira suala zima la ujagina wa mwanamke katika tamthilia hii.

ii) Kudadisi changamoto na mafanikio ya kuujenga ujagina wa mwanamke katika jamii ya kiubabe dume.

## 1.3 NADHARIA TETE

Utafiti huu utaongozwa na nadharia tete zifuatazo;

i) Mwandishi K. W. Wamitila amefaulu pakubwa katika kuusawiri ujagina wa mwanamke katika tamthilia ya *Pango*.

ii) Kuna changamoto nyingi katika harakati za kujenga ujagina wa mwanamke katika jamii yenye mfumo wa ki-ubabedume

## 1.4 SABABU ZA KUCHAGUA MADA HII

Sababu ya kwanza iliyotufanya tuamue kushughulikia maudhui ya ujagina wa mwanamke ni kwamba wanatamthilia wengi ambao wamezama katika kujadili masuala ya wanawake ya kijinsia hasa kuhusiana na mikakati ya jinsi wanawake wanavyoweza kujikwamua kutokana na uonevu wa kijamii hawajashughulikia swala la ujagina wa mwanamke. Sababu ya pili ni kwamba tukilishughulikia, litakuwa kichocheo kwa wahakiki wengine kulitafitia katika kazi zinginezo.Tatu tunanuia kuwahamasisha wanawake wapiganie haki zao bila kujali taasubi za kiume na mfumo wa ubabe-dume ambao zimewasonga kwa muda mrefu. Nne matatizo mengine yanayowakumba wanawake yamejengeka kwenye misingi ya jinsia yao. Mwanamke amewekwa katika kitengo maalumu cha jamii.Licha ya uonevu huu wa kijamii, mada yetu ya ujagina wa mwanamke katika tamthilia ya *Pango* ya K.W Wamitila itaonyesha kuwa mwanamke ana uwezo sawa na mwanamume katika jamii.

## 1.5 UPEO NA MIPAKA YA TASNIFU

Utafiti huu ni wa kimaudhui na tutashughulikia swala la ujagina wa mwanamke katika *Pango*.ya K.W Wamitila.Tutajadili kwa undani jinsi wahusika na uhusika wao wanavyodhihirisha swala la ujagina wa mwanamke kwa kuwaangazia wahusika wakuu wa kike na kiume. Aidha, tutapigia darubini jinsi mwandishi wa tamthilia hii alivyofaulu au kushindwa kumwasilisha mwanamke kama jagina katika kazi yake. Aidha, tutasoma tamthilia ya *pango*,kazi mbali mbali kuhusu fasihi na kazi nyingine zinazohusiana na fani na ujagina wa mwanamke katika kazi mbali mbali za kifasihi

Pia kwa kuwa waandishi na wahakiki wengine wa tanzu mbalimbali za fasihi wamezungumzia kuhusu wanawake katika jamii, inapolazima tutazitalii kazi hizo ili kuikoleza mada yetu

## 1.6 MSINGI WA NADHARIA

Kwa kuwa utafiti wetu unalenga kuudhihirisha ujagina wa mwanamke katika tamthilia ya *Pango*, nadharia itakayotufaa zaidi ni ile ya Ufeministi. Kulingana na Wamitila (2002), nadharia ni mawazo, mpango, mwongozo au maelezo yaliyowekwa ili kusaidia kutatua au kutekeleza jambo fulani. Pia ni vyema tueleze kuwa nadharia yoyote ile ya kihakiki ni nyenzo tu ya kutusaidia kulifikia lengo fulani. Kila nyenzo huwa na ubora na udhaifu wake. Mahali panaposibu nyenzo fulani huenda pasisibu nyingine kwa sababu kila moja ina uwezo wake maalum. Nadharia za kihakiki huathiriana kwa kiasi kikubwa.Wellek (1949) anasema kuwa "hamna nadharia inayoshuka kutoka mbinguni na kudai kuwa na ubunifu."

Nadharia itakayoongoza tasnifu yetu ni Ufeministi. Ufeministi ni dhana inayotokana na neno la Kilatini "Femina" lenye maana ya mwanamke. Dhana hii inarejelea uwakilishaji wa haki za mwanamke kufuatana na kuambatana na imani ya usawa wa kijinsia. Huu ni mwamko wa wanawake kwa njia zote. Bunch (1981) anaonelea kwamba, nadharia ya Ufeministi inajishughulisha na mabadiliko yanayolenga kuunda upya jamii kuhusu nafasi ya mwanamke. Hivyo anaonelea kuwa nadharia hii hutumiwa kwa upana wake kurejelea mwelekeo wa yeyote anayetambua, kung'amua na kujitahidi kukomesha ukandamizwaji wa wanawake.

Kulingana na Engels (1884) mabadiliko yaliyotokea na yenye ustaarabu ndiyo yaliyosababisha udhalimu wa wanawake. Jamii asilia ilikuwa na utathimini sawa wa kazi za wanaume na wanawake. Baadaye mabadiliko ya ustaarabu yalianzisha urithi wa upande wa baba, haya yalitokana na hali ambako kazi za wanawake za uwindaji na ufugaji zilipoanza kuleta faida zaidi kuliko kazi za nyumbani. Ongezeko la mali upande wa baba ni jambo lililozusha kuwepo kwa mali ya kibinafsi na hivyo wanawake wakaanza kuwategemea wanaume kiuchumi.

Mkabala wa kuumeni umetawala jamii nyingi za kilimwengu kwa muda mrefu, jambo hili limesababisha kupuuzwa kwa haki za wanawake kama viumbe kamili. Kauli za kidini na kitamaduni zimetumiwa kushadidi uwezo wa wanaume na kuwadunisha wanawake. Nadharia hii inakinzana na Mikabala ya kuumeni inayoonekana kuwapendelea wanaume na kuwanyanyasa wanawake. Japokuwa kuna mielekeo mingi katika nadharia hii,pametokea sifa mahsusi zinazofafanua nadharia hii. Baadhi ya sifa hizi ni kuwa

(a) Ni nadharia inayotumia fasihi kama jukwaa la kuelezea kwa uyakinifu hali inayomkumba mwanamke

(b) Nadharia hii inanuia kuwasawazisha wanadamu kwa upande wa utamaduni na kimenke.

(c) Mtazamo huu aidha unajaribu kuwahamasisha watungaji wa kazi za sanaa wawe na wahusika wa kike ambao watakuwa vielelezo, wenye uwezo na wanaoweza kuigwa

(d) Ni nadharia inayokuza na kuendeleza hisia za umoja wa wanawake kama kundi linalodhulumiwa.

(e) Mtazamo huu una lengo la kuamsha na kuzindua mwamko miongoni mwa wanawake ili wawe watendaji zaidi na washiriki ipasavyo katika ukombozi wao wenyewe.

(f) Nadharia hii inasisitiza umuhimu wa kuvumbua na kuweka wazi kazi za sanaa zilizotungwa na wanawake ambazo zimepuuzwa kwa sababu ya utamaduni unaompendelea mwanamume.

Tukirejelea maoni ya wataalamu kama Mbatiah (2000:87) ni kuwa nadharia ya ufeministi inajishughulisha na utetezi wa haki za wanawake dhidi ya ukandamizwaji katika jamii zenye mfumo uliodhibitiwa na wanaume. Wahakiki wa kifeministi kama vile Birke (1986) na Lovenduski na Randall (1993) wanadai kwamba, ufeministi ni dhana inayoelezea hali ya wanawake kujieleza katika jamii, mbali na wanaume wanaounga mkono jitihada za wanawake hao.

Mary Wollstonecraft ndiye anayefahamika kuwa mtaalamu wa kwanza kuyazungumzia masuala ya wanawake kwa utaratibu maalum. Katika kazi yake, *A Vindication of the Rights of Women* (1792) anapendekeza kuundwa kwa jamii mpya iliyo na usawa. Wengine waliochangia pakubwa kuikuza nadharia hii ni pamoja na Virginia Woolf katika *A Room of One's Own* (1929), Germaine Greer – *The Female Eunuch* (1949),Simone de Beauvior – *The Second Sex* (1953) na Kate Millet – *Sexual Politics* (1969) Wahakiki na wanadharia hawa wote wanashikilia kwamba mifumo ya kiume katika asasi zinazojikita katika misingi ya ubabe-dume inamnyanyasa mwanamke na haina budi kupingwa kwa kila njia. Freedman (2002:3) anandai kuwa nadharia ya ufeministi ilianzia Ufaransa na kutiliwa nguvu miaka ya sitini na kushika kasi miaka ya themanini na tisini na baadaye kuenea ulimwenguni. Kuna mwelekeo wa Kifaransa, Kimarekani, Kiingereza na

Kiafrika. Katika utafiti wetu, tutajikita katika mrengo wa mtazamo wa Kiafrika kwani tamthilia tunayoishugulikia imeandikwa katika muktadha na mazingira ya Kiafrika. Katika mtazamo wa Kiafrika wanawake wa Kiafrika wanasisitiza zaidi upinzani dhidi ya utamaduni unaomnyima mwanamke nafasi ya kutekeleza malengo yake. Miongoni mwa vitengo vya utamaduni huu ni:

i) Kutotambuliwa kwa mwanamke kama mzazi wa wanajamii.
ii) Tohara na ukeketwaji wa mwanamke
iii) Kimya cha kulazimishwa
iv) Desturi na mila zinazomdhalilisha kama vile kuonewa kwa mwanamke asiyezaa, ndoa za lazima vita vya kinyumbani n.k

Bressler(2003:150-151)anaugawa Ufeminisiti wa Kimagharibi katika makundi matatu kulingana na mipaka ya Kijiografia.Makundi haya ni: Ufeministi wa Marekani,Ufeministi wa Uingereza na Ufeministi wa Ufaransa Wanawake wa Marekani wanatilia mkazo lugha. Wanadai kwamba wanawake wana namna yao ya kipekee ya kuandika kujieleza. Pia wanasema kwamba kuna dhamira zinazorudiwarudiwa katika tungo za wanawake. Wanashughulikia kazi za fasihi zilizotungwa na wanawake kwa wanaume maadamu zinazoongea juu ya wanawake

Wanawake wa Uingereza nao wanaiona dhima yao kuwa ya kisiasa. Wanafikiria kwamba, wenzao wa Kimarekani wanazungumzia zaidi maswala ya kihisia na kisanaa na kusahau historia na siasa. Kwao, mambo ya kihistoria, kisiasa ndiyo huathiri matendo ya wanawake.

Wanawake wa Kifaransa wanatilia mkazo lugha. Utafiti wao unalenga katika kufafanua namna lugha inavyomtolea maana mtumiaji wake. Wanadai kwamba lugha kama inavyotumika ni zao la taasubi ya kiume. Inampendelea mwanamume zaidi kuliko mwanamke. Jazanda zenye kuelezea uwezo, nguvu na mamlaka ni za kiume na ilhali zile zenye kusawiri ulegevu na kutoweza ni za kike.Toril Moi katika *Sexual Politics* (1978) anaeleza kuwa mwana Ufeministi wa Kifaransa, Helene Cixous, ameathiriwa na Jacques Derrida na Jacques Lacan( mwanafunzi wa Derrida). Athari hizi zinatokeza katika mawazo ya ki-uwili kuelezea misingi ya itikadi ya kiume katika jamii. Kwa mfano:

| Mwanamume(ubabe) | | mwanamke(upole) |
|---|---|---|
| Jua | _ | Mwezi |
| Baba | _ | Mama |

Licha ya shutuma kali wanazozitoa baadhi ya wanafeministi kuhusu itikadi hiyo ya kiume, baadhi ya mikabala yao inaelekea kuonyesha itikadi hiyo au kuathiriwa kwa kiasi kikubwa kwa wana nadharia hao na mawazo ya wana nadharia wa kiume. Moi anadokeza kuwa mawazo ya Mary Wollstonecraft yanaathiriwa na mawazo ya kiume yanayohusishwa na mapinduzi ya Ufaransa. Simone de Beauvoir kwa upande wake anaathiriwa sana na Jean Paul Sartre. Licha ya kuwako kwa mikabala tofauti ya nadharia ya Kifeministi, kuna sifa zinazoihusisha mikabala hii na kuifanya kuwa kitu kimoja kiasi cha kuitambua kama nadharia moja mahsusi. Sifa ya kwanza inahusiana na mtazamo kuuhusu utamaduni wa kimagharibi na wa jamii nyinginezo. Utamadunni huo unatazamwa kama unaoelemea upande wa kiume. Huu ni utamaduni unaomkweza mwanamume huku ukimtweza mwanamke. Utamaduni huu unapitisha na kuwarithisha wanajamii wake thamani hizo ambazo zinajitokeza kwenye sanaa na lugha yake.

Pili, utamaduni umeundwa au kujengwa kwa namna inayomkandamiza mwanamke katika nyanja zote za maisha. Wanawake wanapokua na kukulia katika jamii zao,wanayachukua mawazo yanayoendeleza itikadi hii hasi na kwa njia hii kuidharau jinsia yao wenyewe. Kwa mawazo ya Louis Althusser, mwana- Umarx wa Kimuundo wa Ufaransa, tunaweza kusema kuwa wanawake" wanarengwa" na kuyakubali mawazo ya itikadi ya kiume na hata kuyaona kama yao.

Christopher Miller,katika kazi yake,*Theories of Africans* (1990)anataja na kuueleza Ufeministi wa Kiafrika hasa ule unaohusishwa na fasihi.Anatofautisha Ufeministi wa Kimagharibi kwa sababu unajikita katika uhalisi wa mambo ya Kiafrika. Kimsingi,Ufeministi unajishughulisha na uhalisia wa maisha ya mwanamke katika miktadha ya kijamii,kitamaduni na kiuchumi. Ufeministi wa Kiafrika unajishughulisha na haja ya kutaka kuonyesha jinsi miktadha hii inavyochangia kumnyanyasa, kumdunisha na kumdhalilisha mwanamke wa Kiafrika. Licha ya tofauti zake za kijiografia,nadharia ya Kifeministi inaelekea kuafikiana kwenye maswala na malengo fulani ya kimsingi. Fasihi inayojali kipengele cha Ufeministi inafaa kutimiza malengo yafuatayo:

i. Itumike kama jukwaa kwa mwanamke na kueleza kwa uaminifu tajriba ya mwanamke.
ii. Isaidie kuleta usawa wa kitamaduni na kijinsia kwa wanadamu bila kujali maumbile
iii. Iwasawiri wahusika ambao ni vielelezo na wanaoweza kuigwa kwa kuwaumba wanawake wanaojitegemea katika maisha.
iv. Ikuze na kuendeleza hisia za umoja wa wanawake kama kundi linalodhulumiwa.

v. Izindue na kuanzisha mwamko kwa wanawake kwa kuwaonyesha hali halisi kuhusu hadhi ya mwanamke.(Eagleton, 1986:172-174)

Mwasisi wa Ufeministi wa Kiafrika ni Filomena Steady (1981). Steady anaeleza kwamba, Ufeministi unapohusishwa na fasihi ya Kiafrika, unatarajiwa kuchunguza hali za kijamii na kitamaduni zinazochangia unyanyaswaji wa wanawake wa Kiafrika. Anaendelea kudai kwamba, mwanamke wa Kiafrika ni mtetezi wa haki na usawa wa wanawake kuliko mwanamke wa Kimagharibi,kwa kueleza kwamba;

> Ufeministi wa kweli ni ile hali
> ya kujinyima ulinzi wa kiume
> na jitihada za kuwa na busara na
> uwezo wa kujitegemea (uk.35-36).

Kulingana na Steady (1981:30-37), Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika ina sifa zifuatazo:

I. Inatambua uhusiano wake na ufeministi wa kimataifa lakini inafafanua ufeministi ambao una mahitaji na malengo maalum yanayotokana na uhalisi wa maisha ya wanawake katika jamii za Kiafrika .

II. Inatambua kuwa kabla ya ukoloni, katika jamii za Kiafrika, kulikuwa na watawala na mashujaa wanawake.

III. Inaheshimu uwezo wa mwanamke wa Kiafrika wa kujitegemea na kupuuza unyanyaswaji wa utumwa unaomkabili.

IV. Inachunguza hali za mwanamke katika jamii ambazo zimekuwa na vita vya ukombozi wa kitaifa na ujenzi mpya wa jamii zenye usawa wa kijinsia.

Steady anashilikia kuwa wanawake wa Kiafrika pamoja na matatizo mengi yanayowakabili,yalitokana zaidi na utamaduni wa Kiafrika, wao wenyewe walichangia pakubwa katika ule unyanyasaji uliowakabili. Yaani wanawake wa Kiafrika wamekubali kuwa hali na maumbile yao inaruhusu yale wanayotendewa,na kwamba hayo ni majaliwa ya Mungu na hakuna lolote lingeweza kubadilisha hali hii.

Mbali na haya, nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika inatambua kwamba mwanamke wa Kiafrika anaweza kujikomboa na kuishi vyema bila unyanyasaji huu.

Momanyi (1998),anadai kuwa mifumo ya kiumeni ni utaratibu mkubwa wa masharti ambao unachukuliwa kumaanisha kule kuhalalishwa kwa asasi za kijamii zenye kuhimili tofauti za kiuana katika ugawaji wa kazi. Huu ni mfumo ambao unampa mwanamume nguvu dhidi ya mwanamke katika nyanja zote za kimaisha, kisiasa, kiuchumi na kijamii. Katika ugawaji wa majukumu chini ya mfumo huu, wanawake wanapewa nafasi ya pili, baada ya mwanaume. Misingi ya kuwapa wanawake nafasi hii, inafungamanishwa na dini kama dondoo hili la Momanyi linavyoashiria(1998:90);

> Mungu alituumba, wanaume kwa wanawake na kwa sababu
> ya uonevu wa mwanamke, alimjaza mwanamke unyonge wa
> kimwili na wa kiakili. Alimpa mwanaume uzuri wa nguvu, akili na
> mawazo mema, na kutokana na jambo hili, ndipo akawataka
> wanaume wawasimamie wanawake na kuwalinda…..
> Wanawake pia hawana makosa kwa yale wayafanyayo kwani

> hawajui lolote. Lakini makosa yote ni juu ya wanaume wanaojua uzuri
> na ubaya…..

> Kulingana na Ogundipe -Lleslie (1984), ni mwanamke tu ambaye anafaa atambue kuwa yeye ndiye anayeweza kuufasili uhuru wake na kujua kile hasa anachokihitaji.

Mwachofi (1987) Yahya Mulwa (1988) na Said A. Mohamed (2000),wanalipuuza wazo la ndoa kuegemezwa kwenye mali na kumwunga mkono Steady (1981), aliyekuwa katika mstari wa mbele katika kutetea haki za wanawake. Waandishi hawa wanatetea kubadilishwa kwa asasi za kitamaduni zinazomkandamiza mwanamke wa Kiafrika au hata kuzifutilia mbali ili kumthamini mwanamke na kumrejeshea utu na hisia zake za kibinadamu.

Millet (1977), anaeleza kuwa Ufeministu wa Kiafrika uliibuka ili kuwahusisha wanawake katika mawanda mapana ya kijamii miongi mwa jamii za Kiafrika. Kwa hivyo Ufeministu wa Kiafrika husisitiza ugawanaji sawa wa majukumu ya kijamii miongoni mwa wanaume na wanawake.

Strobel (1980), anadai kuwa ijapokuwa Ufeministu wa Kiafrika si mgeni wala uliotulia, umekumbwa na changamoto nyingi kutoka pande mbalimbali. Kwa mfano katika bara la Afrika, kuna wale wanaodai kuwa ufeministi ni tukio ambalo linafaa sana katika mataifa ya magharibi na halina nafasi katika mataifa ya Kiafrika.

Baffoun (1985), anadai kwamba Ufeministi katika Afrika si jambo geni kwa mwanamke wa Kiafrika kwa sababu tangu kuzuka kwa ubabe-dume kumekuwa na pingamiza za kila aina. Kulingana na Carby (1987), Ufeministi wa Kiafrika umejengeka kwenye misingi kuwa wanawake sharti wapewe thamani wazi katika jamii.

Allen (1995) , anadara asasi za kijamii ambazo zimemkweza mwanamume na kumdunisha mwanamke. Allen anaendelea kusema kuwa ufeministi wa Kiafrika huhoji asasi za kijamii ambazo huzuia mwanamke wa Kiafrika kujitambua na kujiamini. Kiini hasa cha kupigania usawa baina ya mwanaume na mwanamke ni kutafuta sauti ya kike, uhuru wa mawazo na vitendo. Pia kumhusisha na kumpa nguvu mwanamke katika maisha ya kila siku. Ufeministi wa Kiafrika siyo tu hudara viunzi vya ubaguzi kwa mwanamke bali pia hupinga unyonyanji wa mwanamke katika jamii inayoongozwa na ubabe-dume.

Diedre (1996), anasema kuwa Ufeministi wa Kiafrika hupigania nguvu sawa baina ya mwanamke na mwanamume na kwamba nguvu na ujike sharti zifungamanishwe bali zisitenganishwe. Pia anadai kuwa nguvu za mwanamke ndizo hukamilisha zile za mwanamume.

Aabbenyi (1997), anasema kuwa lengo la Ufeministi wa Kiafrika ni kujenga jamii inayothamini usawa wa kijinsia na kwamba Ufeministi huu ni muhimu sana kijamii,kisiasa, kiuchumi,kiutamanduni na katika nyanja zote za maisha ya kila siku.

Wafula na Njogu (2007), wanasema kuwa watetezi wa Ufeministi wa Kiafrika wanaamini kuwa udunishwaji wa mwanamke ulitokana na mila na itikadi za Kiafrika. Mila na itikadi hizi hugawa majukumu ya mwanamume na mwanamke katika jamii na kwamba majukumu haya humpendelea mwanamume kuliko mwanamke. Kwa hivyo, Ufeministi wa Kiafrika hupania katika kumpa mwanamke uhuru dhidi ya asasi kandamizi zinazoongozwa na ubabe-dume na matokeo yake yawe ni kumpa mwanamke ushirikishwaji usiodhibitiwa katika nyanja zote za kijamii. Kwa ufupi Wafula na Njogu wanasema kwamba watetezi wa Ufeministi wa Kiafrika wana lengo la kudhihirisha

juhudi zilizoanzishwa na mwanamke wa Kiafrika za kutathmini na kudai nafasi yake katika jamii ya Kiafrika.

## 1.7 YALIYOANDIKWA KUHUSU SOMO HILI

Suala la wanawake katika fasihi ya Kiswahili ni pana. Waandishi na wahakiki mbalimbali wamelizungumzia kwa njia na kwa ufanisi tofautitofauti. Penina Muhando kwenye tamthilia zake *Tambueni Haki Zetu* (1972), *Talaka si Mke* wangu (1976), *Nguzo Mama* (1982) na *Lina Ubani* (1984), amezungumzia kuhusu mwanamke na ukombozi wa mwanamke. Kwenye tamthilia ya *Kilio Cha Haki* ya Alamin Mazrui, ameelezea jinsi mhusika mkuu Lanina anavyodhulumiwa katika shamba la Delamon. Kunakuwa na mapambano kali baina ya wafanyikazi na udhalimu wa Makaburu walioivamia nchi yao. Katika mapambano hayo wanaongozwa na mwanamke jasiri aliyejikomboa kimawazo,ambaye anadhihirisha udhalimu wa jumuiya yake unaowapata wafanyikazi kwa upande mmoja na wanawake kwa upande mwingine. Mhusika mkuu Lanina anafualu katika kuwazindua wafanyikazi wenzake wapambane na udhalimu na watetee haki zao. Mapambano haya yanaleta mwamko wa kisiasa ambao ndio mwanzo wa matayarisho ya vita vilivyokomboa nchi nzima kutokana na ukoloni.

Wamitila K.W.(2003),anasema nadharia ya Ufeministi iliwekewa msingi wake na msukumo wa nia ya kupigania ukombozi wa mwanamke kutokana na pingu za kitamaduni, kijamii, kidini, kisiasa na kiuchumi. Nadharia hii inadadisi msimamo na itikadi za kiume ambazo zimekuwapo kwa muda mrefu zinazoshabiki ubabe-dume.

Lanina amejikomboa kimawazo na ndiposa anafaula katika kuwaongoza wafanyikazi wenzake dhidi ya ubabe-dume unaodhihirishwa na Wakoloni wanaongozwa na Delamon-Kaburu mwenye shamba.

Mbatia, M (2002), anaelezea Ufeministi wa Kiafrika kuwa nadharia ya kifasihi ambayo kazi yake kuu ni kutetea haki za wanawake dhidi ya ukandamizwaji katika jamii iliyo na mfumo uliodhibitiwa na wanaume. Kwenye *Kitumbua kimeingia Mchanga* (2000) ya Said A. Mohamed, Suala la unyanyasaji wa mwanamke limezungumziwa. Said A. Mohamed katika *Kitumbua Kimeingia Mchanga*, anamlika tofauti zilizoko baina ya mila na tamaduni za kale na za kisasa kuhusu swala la ndoa. Ameshughulikia uhuru wa vijana wa kileo kinyume na matakwa ya wazee wao. Hidaya, msichana ambaye Fikirini anataka kumuoa, anatuhumiwa kuwa ni kiruka njia, mhuni na mwovu na wazazi wa Fikirini.

De Beauvior, (1952),katika kitabu cha,*The Second Sex*,anaonyesha mwanamke alivyodunishwa katika asasi ya ndoa, dini na utamanduni ambapo huchukuliwa kama msaidizi wa mwanamume na kwamba mwanamume ndiye anayepaswa kuchagua mpenziwe. Anaendelea kusema kuwa ndoa imejengwa kwenye misingi na imani ya uwezo mkubwa alionao mwanamume akilinganishwa na mwanamke.

Lungano (1989),katika tasnifu yake alishugulikia mwanamke katika riwaya za Kezilahabi. Kazi hizi zimemsawiri mwanamke kwa njia hasi na kuwa yeye ni chombo tu cha kumfurahisha mwanamume. Kwa jumla kazi tulizozitaja hapo juu ni muhimu katika uchunguzi wetu kwani zitakuwa kama mihimili ya utafiti wetu japo kwa uangalifu mwingi tuzije tukapotoka katika utafiti wetu.

Kiango (1992) anaangalia taswira ya mwanamke katika tamthilia za Kiswahili za Kenya. Anasema kuwa mwanamke amesawiriwa kama kiumbe ambaye ni kama chombo cha mwanamume cha kujitajirisha na kuyatimiza mahitaji yake ya kimwili. Mwanamke anasawiriwa kama mbaya, mzinifu, mwaviaji wa mimba na mtu asiye na mwelekeo thabiti.

Kiango anapoihakiki tamthilia ya *Kilio Cha Haki* anaonelea kuwa mwanamke amepewa nafasi ya kipekee kwa sababu mkabala wa Mazrui ni tofauti na mikabala ya waandishi wengine wanaowabeza na kuwakashifu wanawake. Mazrui amemsawiri muhusika Lanina kama mwanamke jasiri, aliyejikomboa kimawazo, ambaye anadhihirisha udhalimu unao wapata wafanyi kazi kwa upande mmoja na wanawake kwa upande mwingine. Hakika, wanawake wameathiriwa na mifumo mbalimbali ya kijamii ambayo ni ya kidini, kiuchumi, kisiasa n.k.

Uchunguzi huu utafaa sana kwani tutashughulikia ujagina kama unavyojitokeza kupitia wahusika katika hali hizo mbalimbali na mifumo ya kijamii. Momanyi (1998), ameshughulikia usawiri wa mwanamke Mwislamu wa jamii ya Waswahili katika ushairi wa Kiswahili. Katika uhakiki wake, Momanyi ameshughulikia usawiri wa mwanamke katika *Utenzi wa Mwana Kupona* . Momanyi anadai kuwa sababu kuu inayochangia udunishwaji wa mwanamke ni dini ya Kiislamu. Momanyi (2001),katika tasnifu yake alishughulikia nafasi ya mwanamke katika *Utubora Mkulima* ya Shaaban Robert.

Elizabeth N. (2006), anaeleza kuwa wanawake wamedhulumiwa katika viwango mbalimbali. Anasema kuwa asasi za jamii zinachangia katika kumkandamiza mwanamke. Kazi tulizozitaja hapo juu ni muhimu kwani zitaonyesha jinsi asasi

mbalimbali za kijamii zinavyowekea vikwazo ujagina wa mwanamke katika *Pango*. Aidha kazi hizi zimejikita sana katika upembezwaji na unyanyasaji wa mwanamke. Utafiti wetu utapiga hatua kadhaa zaidi na kuonyesha ujagina wa mwanamke katika tamthilia ya *Pango*.

## 1.8 NJIA ZA UTAFITI

Utafiti wetu utajikita katika maktaba. Tutasoma tamthilia ya *Pango* ya K.W Wamitila kwa kina kupitia mtazamo wa nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika. Hali kadhalika tutadurusu vitabu vya kifasihi, tasnifu na makala mbalimbali yanayohusiana na mada yetu. Aidha tutarejelea tovuti mbalimbali kwenye mtandao ili tujifahamishe masuala mbalimbali yanayowahusu wanawake hasa yale yanayogusia suala la ujagina wao. Vilevile tutawashirikisha wahadhiri na wasomi wenzetu wenye ujuzi katika mada hii.. Baada ya kukusanya data, tutachanganua na kuwasilisha matokeo ya utafiti wetu kwa njia mwafaka.

# SURA YA PILI

# UJAGINA WA MWANAMKE NA ASASI ZA JAMII

## 2.0 UTANGULIZI

Katika sura hii, tutaelezea dhana ya ujagina kama inavyoelezwa na makamusi na wataalamu mbalimbali kwa kujikita katika matapo matatu ya ujagina: Jagina chanya, jagina hasi/ danganyifu, jagina pwaya/ kinzani. Aidha tutazifafanua sifa mbalimbali za ujagina, na mwisho tutazichambua kwa kina asasi tatu za kimsingi ambazo kulingana na wafeministi wa Kiafrika, ndizo vikwazo vikubwa katika kuudhihirisha ujagina wa mwanamke wa Kiafrika katika kazi za sanaa. Asasi hizi ni: Dini, ndoa na elimu.

## 2.1 Dhana ya Ujagina

Kulingana na Wamitila (2003), jagina au neno "Shujaa", hutumika kuelezea mhusika mkuu katika kazi ya kifasihi ambaye anaweza kuwa wa kike au wa kiume. Kimsingi neno hili haliashirii wema tu. Mhusika mkuu anaweza kuwa mbaya kama alivyo daktari Mtoga katika *Vipuli vya Figo* ya E.Mbogo. Kulingana na Kamusi ya Karne ya 21, inaelezea kuwa jagina ni mtu mwenye ujasiri, mtu awezaye kukabili mambo ya hatari bila hofu. Kamusi ya Kiswahili Sanifu inaelezea kuwa jagina ni mtu mwenye moyo thabiti anayeweza kukabili mambo hata kama ni ya hatari, bila hofu. Kamusi ya shule za Msingi inaelezea kuwa jagina ni mtu hodari aliye na moyo imara wa kutenda mambo hata kama ya hatari kubwa; mtu asiyeogopa; jasiri. Tukijumlisha fasili hizi zote tunaweza kusema kuwa, jagina ni mtu; wa kike au kiume ambaye ni binadamu wa kawaida lakini anayetenda matendo mbalimbali hata kama ni ya hatari.

## 2.2 Aina za Ujagina

Kwa mujibu wa Wamitila (2003)193 kuna aina mbalimbali za ujagina: Jagina chanya, Jagina hasi, Jagina pwaya/ kinzani.

### 2.2.1 Jagina Chanya

Huyu ni jagina anayehusishwa na kazi zilizoandikwa katika misingi ya uhalisia wa kisoshalisti. Wahusika wa aina hii wanapaswa au walipaswa kuwa vielelezo kwa wasomaji, wanaoweza kuwatia hamasa ya kushiriki katika mapinduzi ya kuboresha hali ya jamii. Mhusika wa aina hii ni Pavlov katika riwaya ya Maxim Gorky iitwayo *The Mother*. Mhusika mvita katika Riwaya ya S.A. Mohamed ya *Kiza katika Nuru* ni mfano mwema katika fasihi ya kiswahili.

### 2.2.2 Jagina Hasi/Danganyifu

Huyu ni jagina anayejifanya kuwa ametimiza mambo ambayo kwa kweli yametimizwa na jagina hasa, yaani sio yeye. Hutumiwa pia kuelezea jukumu mojawapo analoweza kulichukua mhusika katika kichimbakazi kwa mawazo ya Vladimir prop katika kitabu chake *The Morphology of the Folktale*. (1968)

### 2.2.3 Jagina Pwaya/Kinzani

Dhana hii hutumiwa kumrejelea mhusika ambaye anatofautiana na jagina kama tunavyomwelewa katika kazi ya kifasihi. Sifa anazokuwa nazo jagina pwaya hupingana na sifa za jagina wa kawaida. Kimsingi jagina pwaya hufanikiwa katika majukumu yake na hufikia kiwango fulani cha ufanisi. Aidha jagina huyu haelekei kutangamana na jamii yake, ni dhaifu na huishia kuonyesho sifa za ushinde. Aghalabu wahusika wanaowekwa katika kundi hili wanahusishwa na waandishi wa kiubwege kama Samuel Beckett na

Eugene Ionescu. Katika fasihi ya Kiswahili sifa za aina hii zinatokeza katika tamthilia ya *Amezidi* ya S.A Mohamed. Wahusika wanaopatikana katika tamthilia za aina hii huweza kujitokeza katika sura mbalimbali, kubadilisha hata jinsia, masuala ya maonyesho hayatiliwi maanani, mfuatano wa kiwakati unapuuzwa na mpaka uliopo kati ya uhalisi na utohalisi huvunjwa. Ni dhihirisho la athari za uhalisiafifi. Mfano wa kazi ya aina hii ni *Upotevu* ya Njiru Kimunyi. Kazi za aina hii pia huwa na wahusika – wasimulizi ambao hawana sifa za kijagina kama za wahusika wa aina yao katika fasihi nyingine.Mfano mzuri ni Kazimoto katika Riwaya ya E. Kezilahabi ya *Kichwamaji.* Baada ya kupambanua aina mbalimbali za ujagina na sifa za kila mmoja wazo, utafiti wetu utajikita katika ujagina chanya ambao unawafaa wahusika waliomo katika *Pango*.

**2.3 Sifa za Ujagina**

Kabla ya kuzaliwa kwa jagina huwa kuna utabiri. Kwa mfano kuzaliwa kwa Nabii Isa. Jamii huwa na misukosuko mingi hadi pale jagina anapozaliwa. Mara nyingi ujana wa jagina haufafanuliwi. Wakati wa kupatikana mimba ili jagina azaliwe huwa na miujiza na vilevile katika kuzaliwa kwake.Jagina hupata majina mengi miongoni mwa jamii yake watu wengi hawamwelewi. Akiwa mtu mzima jagina huwa na maadui wengi na hivyo basi maisha yake huwa hatarini kila wakati. Kwa sababu hii jagina hutorokea sehemu mbalimbali kuepukana na hatari hizi. Maisha ya jagina huwa ni ya kusafiri na anaporudi, huletea jamii yake zawadi. Motifu za safari na zawadi huwa ni muhimu ili kupata ushawishi miongoni mwa wanajamii. Jagina aghalabu hafi kwa magonjwa, yeye huamua kufa kwake na kufufuka kwake. Kufa kwake huzusha mambo ya kimiujiza na ya kiajabu. Kaburi la jagina mara nyingi huwa halijulikani na wanajamii na huwa ni swala la mjadala miongoni mwa wanajamii.

Mtoto jagina anapozaliwa huwa ni tishio kwa Jamii nzima na mara nyingi hutupwa. Mfano ni katika *Mfalme Edipode* Aghalabu anayemsaliti jagina huwa ni mke wake, mpenzi wake, sahibu wake, mtoto wake, mfano, shujaa Liyongo aliyesalitiwa na mwanawe Moni baada ya kupanga njama na Mfalme Mringwari. Anayemsaliti shujaa huharibikiwa na maisha baadaye. Kwa mfano Moni baada ya kumuua baba yake Liyongo, hakupata chochote kama alivyoahidiwa na Mfalme Mringwari baadala yake alifukuzwa kama mbwa. Judasi baada ya kumsaliti Nabii Isa aliharibikiwa na maisha na hatima yake ikawa ni kujitia kitanzi. (Matendo ya Mitume 1: 17-19) Sifa nyingine ya jagina ni kwamba hufa kutokana na sehemu moja ya mwili wake ambayo huwa siri yake.Mfano Lwanda Magere siri ilikuwa kivuli chake, Samsoni-nywele zake n.k. Jagina vilevile huwa na nguvu za kiajabu na aghalabu huwa hana wakati wa kushughulikia familia. Maisha yake huwa ni ya ukinzani. Majagina wengi katika jamii za Kiafrika na katika fasihi ya Kiswahili huwa na mihimili ya kiubabe-dume na huhusu wanaume

## 2.4 Asasi za Jamii

### 2.4.1 Asasi ya Dini

Kulingana na *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* Toleo la tatu Oxford, dini ni imani inayohusiana na mambo ya kiroho, kwamba kuna muumba ambaye aliumba ulimwengu huu na kwamba ndiye mtawala wa kila kilichomo. Dini pia inafasiliwa kama mfumo fulani wa imani na njia ya kuabudu, kusali na kuheshimu/ kutii huyo muumba. Dini ni asasi ambayo inachangia pakubwa katika kuendeleza mfumo wa kibabedume. Dini hufanya hivi kwa kumpa mwanamume mamlaka halisi kama kiongozi wa familia yake. Millet anasema:

> Ushirikiano kati ya familia na jamii kwa
> jumla ni muhimu katika mfumo wa
> kibabedume. Hii imepelekea jamii
> kuunga mkono misimamo ya kidini
> kama vile ile ya dini ya kikristo kuwa
> mwanamume ndiye kiongozi wa
> familia yake.(Waefeso 5:21)

Mtaalamu huyu anaendelea kufafanua jambo hili kwa kusema kuwa, ubabedume unaungwa mkono na Mungu. Mafundisho ya kidini huchangia pakubwa kuupa nguvu mfumo wa ki-ubabedume. Mafundisho hayo ya kidini humsawiri mwanamke kama kiumbe hatari na asili ya maovu yote.

Dini, hivyo basi, inasaidia sana kuendeleza mfumo wa ki-ubabedume. Tumeeleza kuwa dini inahusu imani. Wafuasi wa dini fulani huzingatia maandiko matakatifu ya dini yao bila kupinga jambo lolote. Mtu ambaye anapinga mafundisho ya dini fulani husemekana amepoteza njia. Kwa hivyo, dini inapofundisha kuwa mwanamume ndiye kiongozi wa familia, wafuasi wake hawana budi ila kufuata na kutekeleza mafundisho hayo. Mwanamke anapojaribu kujikwamua kutokana na dhuluma ya mumewe, hukumbushwa kuwa dini inafundisha kuwa mke amtii mumewe. Mwanamke hulazimika kumtii mumewe kwa kuchelea kuwa iwapo hatamtii, atasemekana kuwa hafuati mafundisho ya kidini. Kwa upande mwingine, maandishi mengi kuhusiana na dini, yaliandikwa na wanaume. Dini iliupa ubabedume nguvu nyingi na mwanamke akadhalilishwa zaidi.

Taswira ya mwanamke katika dini kadhaa inadhihirisha jinsi mwanamke alivyodhalilishwa. Hivi ndivyo hali ilivyo katika dini ya Kiislamu. Kurani Takatifu inasema:

> Na waambieni waaminio wanawake wainamishe macho yao, na wazilinde tupu zao, wala wasidhihirishe mapambo yao isipokuwa yale yaliyodhihirika katika hayo. Ila kwa waume wao au baba yao au baba ya waume wao, au wana wao, au wana wa waume wao, au kaka yao, au wana wa kaka yao, au wana wa dada yao, au wanawake wao, au wale iliyowamiliki mikono yao ya kuume, au watu wafikao mara kwa mara wasio watamanifu katika waume, au watoto ambao hawajajua siri za wanawake, wala wasipige miguu yao ili wajulikane wanayoyaficha katika mapambo yao. Na tubieni nyote kwa Mwenyezi Mungu, enyi waaminio, ili mpate kufaulu. (Sura 24: 32).

Mwanamke amedhalilishwa kiasi cha kuwekewa mipaka ya nini la kufanya, kipi cha kuvaa, namna ya kutembea na kadhalika. Mambo haya yote yanadhihirisha jinsi dini inavyochangia kuendeleza ubabedume. Maoni haya ya asasi ya dini kuchangia katika kuendeleza ubabedume yameungwa mkono na De Beauvoir (1949) anayesema:

> Mafundisho ya dini ya kikristo yamechangia
> kuendeleza ubabedume. Katika Agano Jipya,
> Paulo alifunza kuwa mwanamke aliumbwa
> ili kumtumikia mwanamume.(Mwanzo 2:24)

Dini inachangia kuendeleza mfumo wa ki-ubabedume pia kwa kuidhinisha asasi ya ndoa ambayo kama tulivyoeleza hapo chini, imechangia sana kuupa nguvu mfumo huu wa ki-ubabedume. Zeba (1976:35) anasema:

Dini ya Kiislamu hushikilia kuwa,

ndoa ni asasi ya kijamii na Waislamu

wote ni lazima waoe au waolewe

Wanawake wanapoolewa wanajikuta katika familia zinazotawaliwa na wanaume. Kwa hivyo, dini inachangia kuwepo kwa ubabedume kwa kuhimiza waumini wake waoe au waolewe. Watu wanatii dini zao ili kupata ufalme wa milele baada ya kifo na hivyo basi, kuoa au kuolewa. Jinsi asasi ya ndoa inavyozidi kuimarika kupitia kwa asasi ya dini, ndivyo ubabedume unavyozidi kuimarika.

### 2.4.2 Asasi ya Ndoa

Ndoa ni asasi inayoendeleza ubabedume kwa kuwa ndio msingi wa familia. Kupitia kwa familia, watoto wanazaliwa katika jamii na kizazi cha binadamu kinaweza kuendelea kuwepo duniani. Millet (1977) anasema:

Asasi kuu inayoendeleza ubabedume ni ndoa.

Ndoa hupelekea kuwepo kwa familia.

Familia ni kitengo muhimu katika

kuimarika kwa ubabedume kwa kuwa

viongozi wa familia hizo ni wanaume.

Ndoa inauwezesha mfumo wa ubabedume kukita mizizi katika jamii kwa kuwa inapelekea kuwepo kwa familia ambapo mwanamume ndiye kiongozi. Mwanamke anapoolewa hujipata chini ya uongozi wa mwanamume. Mambo yote anayoyafanya lazima yaidhinishwa na mumewe. Ili mfumo wa ubabedume uimarike vizuri, ni lazima kuwe na mtawala na mtawaliwa. Kwa kutokuwa na ndoa, mwanamume hangekuwa mtu wa kutawala, huenda mtazamo wake kuhusu wanawake ungebadilika

Sababu nyingine ambayo inaifanya asasi ya ndoa kuendeleza ubabedume ni majukumu ambayo mwanamke amepewa katika asasi hiyo. De Beauvoir (1985) anasema:

> Asasi ya ndoa imempa mwanamke majukumu
> mawili muhimu. Kwanza, ni kuzaa watoto
> na pili ni kuhakikisha kuwa anatimiza
> mahitaji ya kimapenzi kwa mumewe na
> kuangalia nyumba yake.

Maoni haya yanaungwa mkono na Seif-al-Hatimy (1979) anayesema kuwa sababu kuu ya ndoa ni kupata watoto. Kulingana na maelezo haya ndoa inachangia pakubwa kuendeleza ubabedume. Mwanamke anatakiwa kukidhi mahitaji ya mwanamume ya kimapenzi na kulinda nyumba yake. Hakuna usawa wowote hapa. Huku ni kumdhulumu mwanamke, kwa nini mwanamke awe ndiye atakayekidhi mahitaji ya mwanamume? Je, hii ina maana kuwa mwanamke hana mahitaji? Kwa kusema kuwa mwanamke anapaswa kulinda nyumba, tunapaswa kuelewa kuwa jambo hilo si rahisi kwani mwanamke anatakiwa kufanya kazi nyingi sana nyumbani.Inabidi aamke mapema, afue, apike na awatunze watoto vyema. De Beauvoir (1985) anasema:

> "Kazi ya mwanamke aliyeolewa ni kufua nguo,
> kupangusa vumbi, kung'arisha sakafu
> na kadhalika. Hata hivyo juhudi hizi za
> mwanamke hazifai kitu kwani uchafu daima
> upo. Ndoa inaendeleza ubabedume pia kwa
> kuwa mara nyingi wanawake wanapoozwa
> hawahusishwi katika mipango ya ndoa hiyo

au kuulizwa watoe maoni yao. Wanaume kutoka familia husika (familia ya mwanamke na ya mwanamume) ndio wanaoshiriki mipango ya ndoa". De Beauvoir (1949) anaendelea kusema:

"Wakati wa kuoa, mwanamume hamposi mwanamke moja kwa moja; wanaume kutoka familia husika ndio wanaoshughulikia swala hili. Mwanamke anaishia kujipata katika familia mpya inayotawaliwa na wanaume asiowajua".

Kwa hivyo ubabedume unazidi kutawala na ndoa inaupa nguvu zaidi. Mwanamke anapojipata katika familia hiyo ngeni inayotawaliwa na wanaume wenye mamlaka kamili, hana jingine, ila kutii na kunyenyekea. Katika sherehe ya arusi miongoni mwa utamaduni wa Kidavida, msichana ndiye anayemshika mkono dadake na kumkabidhi kwa bwana arusi. Morgan (1992:47) Anasema,

"Katika utamaduni wa magharibi baba ndiye anayemkabidhi bwana arusi bintiye. Inaaminiwa kuwa kufanya hivi kunamfanya mwanamke kuzaa watoto wa kiume" (1992: 47). Kwa hivyo, ubabedume unapewa nguvu nyingi sana na asasi ya ndoa. Umuhimu wa watoto wa kiume unahimizwa kuanzia siku ya kwanza mwanamke anapoolewa.

Asasi ya ndoa pia inasaidia kuendeleza mfumo wa ki-ubabedume kwa kumfanya mwanamke mtumwa wa mwanamume. Mwanamke analazimika kumtegemea mwanamume kiuchumi kwani hapewi nafasi yoyote ya kujitafutia mali yake. Kama tulivyoeleza hapo juu mwanamke anawajibika kukaa nyumbani na shughuli zake zote ni

za nyumbani. Mwanamume ndiye mwenye uwezo wa kiuchumi. De Beauvoir (1988), anasema, “Katika ndoa mwanamke anapigwa na tabia yake inachunguzwa kwa makini. Jinsi mwanamume anavyokuwa tajiri, ndivyo mwanamke anavyomtegemea zaidi”.Hivyo basi, asasi ya ndoa inapomfanya mwanamke amtegemee mwanamume, inazidi kuupa mfumo dhalilishi wa ubabedume nguvu zaidi. Mwanamke anazidi kuingia katika shimo ambalo kimo chake hakijulikani.

### 2.4.3 Asasi za Elimu

Elimu ni muhimu sana katika maisha ya binadamu. Hata hivyo, mfumo wa ki-ubabedume haumpi mwanamke nafasi ya kupata elimu. Tujuavyo ni kwamba, manufaa ya elimu ni mengi. Hivyo basi mwanamke anapitwa na mambo mengi kwa kukosa elimu. Millet (1969) anasema, “Kama elimu ni nguvu, nguvu pia ni elimu. Sababu kuu ya kufaulu kwa mfumo wa ki-ubabedume ni kuwa unamnyima mwanamke elimu.” Hata pale mwanamke anapopata elimu, elimu hiyo ni duni ikilinganishwa na ile ya mwanamume. De Beauvoir (1952) anasema.”Mwanamke aliishi maisha ya kumtegemea mwanamume. Hakupata elimu muhimu na hakuweza kushiriki kikamilifu katika maendeleo.” Maoni haya yanaungwa mkono na Gerda anayesema, “Wanawake walinyimwa haki ya kupata elimu na hivyo basi, wakaachwa nje katika historia.” Bell na Offen (1977) wanasema kuwa mwanamke hapaswi kupewa elimu sawa na mwanamume. Mwanamume anapaswa kupewa elimu ya juu zaidi. Kupitia elimu, binadamu amejifunza mambo mengi na kuvumbua mengi hasa katika sayansi na teknolojia.

Hapo zamani binadamu alikumbwa na majanga mengi kama vile ukame, mafuriko na magonjwa yasiokuwa na tiba. Baada ya kuelimika na kufanya utafiti, aliweza kusuluhisha

baadhi ya matatizo hayo. Alitengeneza dawa, alinyunyizia mimea maji, na kuhifadhi chakula vizuri ili kimfae wakati wa ukame. Ufanisi huu uliweza kufikiwa kwa kuwa alielewa mazingira yake na kuyatumia ili yamfae. Mambo haya yalifanywa na wanaume. Kwa upande mwingine, mwanamke alidhibitiwa na mfumo wa ki-ubabedume na kutoshirikishwa katika maendeleo haya. Mwanamke alibaki nyumbani na kunyimwa nafasi ya kupata elimu. Hadhi ya mwanamke ikazidi kudhoofika zaidi katika jamii. Kumnyima mwanamke elimu ndiko kumechangia zaidi nafasi duni ambayo amepewa katika jamii. Madai haya yana ukweli mwingi. Wanawake walioelimika huweza kutambua haki zao na kuzidai ilhali baadhi ya wanawake ambao hawakufanikiwa kupata elimu hushindwa kutambua haki hizo.

# SURA YA TATU

## UJAGINA WA MWANAMKE UNAVYODHIHIRIKA KATIKA *PANGO*

### 3.0 UTANGULIZI

Pango (2003) ya K.W. Wamitila inayaangazia matatizo yanayowakumba wanajamii wa nchi ya Pango. Aidha inaumulika mvutano baina ya usasa na ukale. Usasa ukiwakilishwa na vijana wanaongozwa na jagina Katango na ukale ukiwakilishwa na wazee wanaongozwa na Ngwese. Baadhi ya matatizo yanayowakumba wanajamii wa Pango ni pamoja na ya kiuchumi, kisiasa, uongozi mbaya, kitamaduni, ubaguazi, ubabe-dume na ufisadi unaotekelezwa na kizazi cha kale (wazee). Licha ya matatizo haya yote panaibuka jagina mwanamke Katango ambaye anawaongoza vijana katika kulikomboa Pango kutokana na matatizo haya.

Anakumbana na changamoto za kila aina. Kwa mfano, kudharauliwa, kudhalilishwa na dhuluma za kila namna kutoka kwa wazee lakini hatimaye, anafaulu katika kulikomboa Pango.Katika sura hii tutaihakiki tamthilia *ya Pango* (2003) kwa kutumia nadharia ya Ufemisti wa Kiafrika. Tutaonyesha jinsi utamaduni na asasi za elimu zinavyotumiwa na jamii yake kumzuia mhusika mkuu Katango kuudhihirisha ujagina wake kama mwanamke. Vilevile tutaangalia jinsi mhusika huyu anavyokabiliana na vizuizi katika kuudhihirisha ujagina wake. Katika kuyachambua haya, tutaonyesha ujagina wa mhusika mkuu Katango miongoni  mwa wazee na pia miongani mwa vijana. Aidha tutazieleza changamoto zinazomkabili Katango katika kuudhihirisha ujagina huu.

## 3.1 DHIHIRISHO LA UJAGINA WA KATANGO MIONGONI MWA WAZEE

Katika kikundi hiki,kuna wazee kama; Ngwese-ambaye ndiye mpinzani mkuu wa Katango, Seki-babake Katango, Babu-baba yake Ngwese, Ngoi-rafiki yake Ngwese, Malebo-rafiki yake Ngwese umri sawa na Ngoi. Katango ni mwanamke kijana; mwalimu,dadake Susa na Sota. Katika *Pango*, analiongoza kundi la vijana katika kuutwaa uongozi kutoka kwa kikundi cha wazee wanaongozwa na mhusika Ngwese.Katango akishirikiana na kundi la vijana kama vile Kibwana na Kikubi anafanya kila jitihada ili kuutwaa uongozi wa Pango kutoka mikononi mwa wazee hasa Ngwese. Inakuwa ni changamoto kubwa kwake, lakini hatimaye anadhihirisha ujagina wake na kuupata uongozi wa Pango.

Katango anadhihirisha ujagina wake anapochambua hulka ya Ngwese kwa kusema,

> *Ubinafsi umemlevya kabisa uchoyo*
>
> *umevotana na pumzi yake haina*
>
> *inatoka katika kinywa chake…* (uk.9)

Katango anazidi kuudhihirisha ujagina wake kwa kumzomea Ngwese na kumwambia kuwa asidhani angeweza kumtisha kama alivyowatisha watoto alipowapata kisimani(uk 10).Mazungumzo baina ya Ngwese na Katango yanaonyesha wazi kuwa Ngwese ana mtazamo kandamizi dhidi ya mwanamke. Anafanya kila hila kuona kuwa ujagina wa Katango haupevuki. Aidha Ngwese anaamini kuwa ubabe–dume ndio suluhisho la kumzuia mwanamke kuudhirisha ujagina wake(uk 11).

Ngwese anaonekana kuamini kuwa mwanamke hafai kuwa na elimu kama mwanamume. Lakini Katango ameukiuka mtazamo huo wa kitamanduni na kujipatia elimu. Mtazamo huu unaungwa mkono na Bell na Offen katika *The Pedagogy of the Oppressed* (1872), wanaposema kuwa,

> *Mwanamke hapaswi kupewa elimu sawa na mwanamume.*
>
> *Mwanamume anapaswa kupewa elimu ya juu zaidi .(uk.82)*

Katika uk. 12, katango anaendelea kuudhihirisha ujagina wake anapoendelea kujibizana na Ngwese.

Majibizano haya yanadhihirisha kuwa, utamanduni katika *Pango* umemzuia mwanamke kuwa kiongozi. Ufeministi wa Kiafrika unadai kuwa, baadhi ya mambo yanayomzuia mwanamke kuongoza ni utamanduni ambao hutawaliwa na ubabe-dume. Katango amepuuzilia mbali desturi hizo kwa kuonyesha nia yake ya kutaka uongozi wa Pango. Katango anaendelea kukabiliana na Ngwese kwa kumwambia kuwa babake Ngwese alikuwa kibarakala wa wakoloni.

Bunch (1981),anaonelea kuwa, nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika inajishughulisha na mabadiliko yanayolenga kuunda upya jamii kuhusu nafasi ya mwanamke. Hivyo anaonelea kuwa nadharia hii hutumiwa kwa upana wake kurejelea mwelekeo wa mtu yeyote anayetambua, kung'amua na kujitahidi kukomesha ukandamizwaji wa wanawake. Kulingana na Steady (1981:30-37), nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika inaheshimu uwezo wa mwanamke wa Kiafrika wa kujitegemea na kupuuza unyanyaswaji na utumwa unaomkabili. Steady anaendelea kusema kuwa, nadharia hii inachunguza hali za mwanamke katika jamii ambazo zimekuwa na vita vya ukombozi wa kitaifa na ujenzi

mpya wa jamii zenye usawa wa kijinsia. Steady anashikilia kuwa wanawake wa Kiafrika pamoja na matatizo mengi yanayowakabili, yalitokana zaidi na utamaduni wa Kiafrika. Mbali na hayo, nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika inatambua kwamba mwanamke wa Kiafrika anaweza kujikomboa na kuishi vyema bila unyanyasaji huu.

Katango ni jagina anayefahamu historia ya jamii yake. Haya yanadhihirika wakati anapomwambia Ngwese kuwa babake (Ngwese) alikuwa kibaraka wa Wakoloni. Katango anaelezea haya kwa kusema,

*Kwani unadhani yamefichwa*

*na yatafichwaje? Nani asiyejua*

*kuwa alikuwa kibarakala*

*wa Wakoloni?*

Katango anakumbuka vyema ahadi yake na kizazi kipya kuhusu ukombozi wa Pango kwa kusema,

*Sauti ya kizazi kipya inaita sauti ya wanawake*
*waliokuwa mashujaa. Inaita na kulia machozi*
*mekundu ya machwejua na kuuliza. Sote*
*tulikubaliana kwamba tulibebe gogo hili*
*la hatima yetu kwamba tulipagaze*
*mabegani kwa kujitolea lakini tulipofika*
*kati kati ya mto baadhi wakakimbia*
*wakakimbia wengine kuwasaliti*

*wakakimbia wakakimbia na kurudi*

*kuja kulichoma letu pango huku*

*wakishirikiana na adui wa pango…*

*Je, inakuwaje mara hii? Je, watafanyaje*

*mara hii? Je,je..je…?*

Katango anavunja mtazamo wa ki-ubabedume ambao humzuia mwanamke kuzungumza mwanamume anapoongea.

Ubabe-dume unazidi kudhihirika wakati Katango na nyumbani ameshika mata na mishale na kumkuta babake (Seki). Anamkaripia Katango na kumtuhumu kama aliye kwenda kinyume na utamaduni (uk 18)

Simon De Beauvoir (1949), Katika *The Second Sex* anasema kuwa mwanamke wa Kiafrika amefungwa katika pingu za utamaduni zinazomfanya kukubali kudhalilishw/a. Mwanamke anapokubali tamaduni hizo hutumiwa kama chombo cha kuendeleza tamaduni hizo dhalilishi.

Momanyi (1998), anadai kuwa mifumo ya kiumeni ni utaratibu wa masharti ambao unachukuliwa kumaanisha kule kuhalalishwa kwa asasi za kijamii zenye mihimili tofauti za kiuana katika ugawaji wa kazi. Huu ni mfumo ambao unampa mwanamume nguvu dhidi ya mwanamke katika nyanja zote za kimaisha,kisiasa, kiutamaduni, kiuchumi, kijamii n.k. Katika ugawaji wa majukumu chini ya mfumo huu, wanawake wanapewa nafasi ya pili, baada ya wanaume. Misingi ya kuwapa wanawake nafasi hii, inafungamanishwa na dini kama dondoo hili linavyoashiria: Momanyi (1998:90)

*Mungu alituumba, wanaume kwa*

*wanawake na kwa sababu ya uoneva wa mwanamke,*

*alimjaza mwanamke unyonge wa kimwili*

*na wa kiakili. Alimpa mwanamume uzuri wa*

*nguvu, akili na mawazo mema,*

*na kutokatana na jambo hili,*

*ndipo akawataka wanaume*

*wawasimamie wanawake na kuwalinda…*

Kulingana na Ogundipe-Lleslie (1994), ni mwanamke tu ambaye anafaa atambue kuwa yeye ndiye anayeweza kuufasili uhuru wake na kujua kile hasa anachokihitaji.

Seki babake Katango, ni mhafidhina wa utamaduni kandamizi ambao unamzuia Katango kuudhirisha ujagina wake. Haya yanadhihirika wakati Seki anapompata Katango ameshika mata na mishale na kusema,

*Umesikia wapi wewe mwanamke*

*ameshika mate na mishale katika jamii*

*hii? Ehh, niambie hiyo elimu ya kizungu*

*ndiyo iliyokupa ujasiri wa kuipuuza mila?*

Utamanduni unajidhihirisha kama kikwazo kikuu kwa mwanamke anapotaka kuudhihirisha ujagina wake, lakini Katango anaonekana kuupuzilia mbali utamaduni huo uliosheheni ubabe-dume unaomnyanyasa mwanamke kwa kumkabili baba yake na kumwambia kuwa huo ni ushirikina (uk wa 19).

Kulinga na wanajamii wa Pango, utamaduni kandamizi wa ukeketwaji wa wanawake unaendelezwa,kupigwa kwa wanawake na dhuluma nyingine nyingi dhidi ya mwanamke. Katango anatishwa na Ngwese kwa kumwambia kuwa atampapata makofi kama njia ya kumtia adabu. Katango anadhihirisha ujagina wake kwa kukabiliana naye (Ngwese) kwa maneno makali pale Ngwese alipomwambia kuwa, angempapata makofi na kwamba Katango angefaa aolewe ili atiwe adabu na mumewe (uk 14).

Katango katika ukurasa wa 19, anapoulizwa na babake kama alikuwa na mpango wa kumpinga Ngwese ambapo ni kinyume na utamaduni anajitetea kishujaa na kusema kuwa ana haki ya kuwania uongozi kama mwana pango yeyote ule. Kwa kuudhihirisha ujagina huo umekiuka falsafa ya ubabe-dume unaodai kuwa mwanamke hafai kuwa kiongozi.

Katango anamwambia babake Seki kuwa mambo yamebadilika (uk. 20) Bunch (1981) anaonelea kwamba,

> nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika
> inajishughulisha na mabadiliko yanayolenga
> kuunda upya jamii kuhusu nafasi ya mwanamke.
> Anadai pia kuwa mwanamke ndiye adui wa
> Mwanamke mwenzake katika harakati za
> kujikomboa kutokana na minyororo ya mifumo
> wa ubabe-dume (uk. 25).

Mazungumuzo baina ya Kibwana, Kikubi na Mbabekazi yanadhihirisha kuwa, mwanamke ni kizuizi kikubwa dhidi ya mwanamke mwenzake katika kuudhihirisha ujagina. Mbabekazi anaonyesha mtazamo hasi katika uongozi wa Katango kwa kusema,

*Haiwezekani! Culture, Culture Bwana,*

*unafikiri watu watakubali mwanamke*

*awaongoze wewe? We are not yet there!(uk 25)*

Kikubi naye anadakia na kusema,

*Mie nakwambia kila siku! Adui wa*

*mwanamke ni mwanamke Mwenyewe!*

*Unasikia hayo? Unasikia?* (uk 25).

Katango anapokuwa njiani na Kibwana, wanashambuliwa na watu wawili Katango anaudhihirisha ujagina wake anapokabiliana na watu hao bila woga wowote.

Mtu I anapomwamuru Katango asipige kelele, Katango anampuuza na hata anamwendea kutaka kumvua vazi alilojifunika. Mtu II anapodai kuwa Katango ni mwoga baada ya kushtuliwa na Mtu I na kujivuta nyuma kidogo, Katango anasimama kidete na kusema,

*Ndiyo waoga nyie, mjifumbao*

*nyuso na kuuficha ukatili wenu!*

*Ehh mnafumbia nini hapo ila unyama?*

Taasubi za kiume zinadhihirishwa na mtu I anayedai kuwa Katango ni mwanamke tu. Dhuluma nyingi zinazowakabili wanawake hutokana na jinsia yao. Dhuluma hizi huzuia ujagina wa mwanamke kujitokeleza katika maswala mengi ya kijamii. Katango amejikaza kisabuni na kukabiliana na dhuluma hizi.

Mary Wollstonecraft katika kazi yake ya *A Vandication of the Rights of Women* (1792), anapendekeza kuundwa kwa jamii mpya iliyo na usawa. Kate Millet katika kazi yake ya

S*exual Politics* (1969), anashikilia kwamba mifumo ya kiume katika asasi zinazojikita katika misingi ya ubabe-dume inamnyanyasa mwanamke na haina budi kupigwa kwa kila njia. Filomena Steady (1981), anaeleza kwamba, Ufeministi unapohusishwa na fasihi ya Kiafrika, unatarajiwa kuchunguza hali za kijamii na kitamaduni zinazochangia unyanyaswaji wa wanawake wa Kiafrika. Anaendelea kudai kwamba, mwanamke wa Kiafrika ni mtetezi wa haki na usawa wa wanawake kuliko mwanamke wa Kimagharibi, kwa kueleza kwamba,

> Ufeministi wa kweli ni ile hali ya kujinyima
>
> ulinzi wa kiume na jitihada za kuwa na
>
> busara na uwezo wa kujitegemea.(Uk. 21-34)

Majibizano baina ya Katango, Mtu I na Mtu II, yanaashiria kuwa mtu II anaungama kuwa, elimu ina uwezo wa kuvunja tamaduni kandamizi zinazochangia dhuluma dhidi ya mwanamke wa Kiafrika. Katango kupitia elimu yake ameendelea kuudhihirisha ujagina wake.(uk 32)

### 3.1.1 MCHANGO WA VIJANA KATIKA KUUDHIHIRISHA UJAGINA WA KATANGO

Katika kikundi hiki, kuna vijana kama; Kibwana-mwanaume kijana; rafiki yake Katango, Mbabekazi-msichana; rafiki yake Kikubi, Kikubi-mwanamume kijana. Katika nchi ya Pango kuna matatizo ya kisiasa, kiuchumi, uongozi mbaya na ufisadi yote haya yanaendelezwa na kizazi cha kale kinachoongozwa na mhusika Ngwese. Katango anajitoma kwenye siasa kupigania uongozi wa Pango. Anashirikiana na vijana tuliowataja ili kuyalete mageuzi.

Katango anakumbana na changamoto nyingi za kiutamaduni zisizomruhusu mwanamke kuongoza katika jamii ya kiubabe-dume, Strobel (1980), anadai kuwa ijapokuwa Ufeministi wa Kiafrika si mgeni wala uliotulia, umekumbwa na changamoto nyingi kutoka pande mbalimbali. Kwa mfano, katika bara la Afrika, kuna wale wanaodai kuwa Ufeministi ni tukio ambalo linafaa sana katika mataifa ya magharibi na halina nafasi katika mataifa ya Kiafrika.

Baffoun (1985), anadai kwamba, Ufeministi katika Afrika si jambo geni kwa mwanamke wa Kiafrika kwa sababu tangu kuzuka kwa ubabe-dume kumekuwa na pingamizi za kila aina. Kulingana na Carby (1987), Ufeministi wa Kiafrika umejengeka katika misingi kuwa wanawake sharti wapewe thamani wazi katika jamii.

Hotelini ambamo Kibwana, Kikubi na Mbabekazi wamekutana, wanazungumzia kumhusu Katango. Kibwana anawasimulia kuhusu makala kwenye gazeti ambayo inaelezea nia ya Katango kuliongoza Pango.

Kikubi katika mazungumzo haya anadhihirisha kuwa ujagina wa Katango ulianza tangu walipokuwa wakisoma pamoja kwa kusema,

*Ahh huyo? nimesoma naye…*

*aliwahenyesha wanaume ile*

*mbaya kutokana na misimamo*

*yake. Ana ujasiri sana beibe yule! (uk 25)*

Tunaona kuwa ujagina wa katango ulianza kudhirika tangu alipokuwa

Shuleni. Tunaweza tukadai kuwa katango alizaliwa na karama ya ujasiri na ujagina.

Allan (1995), anagusia asasi za kijamii ambazo zimemkweza mwanamume na kumdunisha mwanamke. Allan anaendelea kusema kuwa, Ufeministi wa Kiafrika huhoji asasi za kijamii ambazo huzuia mwanamke wa Kiafrika kujitambua na kujiamini. Kiini hasa cha kupigania usawa baina ya mwanamume na mwanamke ni kutafuta sauti ya kike, uhuru wa mawazo na vitendo. Pia kumhushisha na kumpa nguvu mwanamke katika maisha ya kila siku .Ufeministi wa Kiafrika sio tu hudara viunzi vya ubaguzi kwa mwanamke bali hupinga unyonyaji wa mwanamke katika jamii inayoongozwa na ubabe- dume.

Diedre (1996),anasema kuwa Ufeministi wa Kiafrika hupigania nguvu sawa baina ya mwanamke na mwanamume na kwamba nguvu na ujike sharti zifungamanishwe bali zisitenganishwe. Pia anadai kuwa nguvu za mwanamke ndizo hukamilisha zile za mwanaume. Filomena steady (1981), anaeleza kwamba Ufeministi unapohusishwa na fasihi ya Kiafrika, unatarajiwa kuchunguza hali za kijamii na kitamaduni

zinazochangia unyanyaswaji wa wanawake wa Kiafrika. Anaendelea kudai kwamba, mwanamke wa Kiafrika ni mtetezi wa haki na usawa wa wanawake kuliko mwanamke wa Kimagharibi. Ni dhahiri kuwa Katango ni mhusika mkuu katika *Pango* anayetetea haki na usawa wa mwanamke wa Kiafrika. Ana imani kuwa atautwaa uongozi wa Pango kwa kusema,

*Ehhh mara hii asali*
*ya Pango ni lazima*
*iwafaidi wote.(Uk.34).*

Katango na mpenziwe Kibwana wanapokuwa njiana wanatembea na kushambuliwa na mtu I na mtu II, Katango anaendelea kuudhihirisha ushujaa wake anapokabiliana na wavamizi hao kwa jino na ukucha. Licha ya kuamrishwa na wavamizi hao anyamaze, anakaidi na kuipaaza sauti juu katika jitihada za kumwokoa Kibwana.

Mugambi (1982), anasema kwamba, mwanamke amebanwa na kupewa sifa za mnyonge asiye na nguvu wala uwezo mbele ya mwanamume. Lakini angali anajaribu kuipinga hali hiyo. Kulingana na nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika swala la ngono limeshughulikiwa tangu awali.Waitifaki wa nadharia hii wanapinga hali ya kuwafanya wanawake kuwa kama chombo cha kukinaiza uchu wa mwanamume katika ndoa au nje ya ndoa.

Aristotle (1998), anasema kwamba wanawake huwa chini ya utawala wa wanaume. Utotoni wanajinyenyekezea baba zao na wanapoolewa hujinyenyekezea kwa waume zao, hali hii ndiyo inayozingatiwa na jamii za Kiafrika. Katika (uk. 36), tunaambiwa kuwa, uwanjani panapofanywa mkutano, kundi la vijana linaloongozwa na Kibwana na linafika likicheza ngoma kwa msisimko mkubwa. Wengine wamembeba juu Katango. Ni wazi

kuwa Kibwana anamuunga mkono Katango kwa kila njia. Anaamini kuwa huu ni wakati wa vijana kuongoza Pango. Anadhihirisha haya kwa kusema,

> Upepo umebadili majira, haya
> ni mengine majira kale iliyokuwako
> imechwewa na jua la ufahamu
> umetuchea, vijana!! Hatutishwi
> na kupigwa kabari ii (uk 36)

Kundi la vijana limeshawishika kuwa Katango ana uwezo wa kuliongoza Pango. Hii ndio sababu wanamwinua juu na kusema Katango oyee.!

Pia ni kweli kusema kuwa mnato, ujasiri na ushujaa wa Katango tayari umewavutia vijana wengi wa Pango. Licha ya vikwazo vingi kutoka kwa wazee wanaongozwa na Ngwese bado ananawiri.(uk 39)

## 3.2 PINGAMIZI NA CHANGAMOTO ZINAZOMKABILI KATANGO KATIKA KUUDHIHIRISHA UJAGINA WAKE

### 3.2.1 UTANGULIZI

Kamusi ya Kiswahili Sanifu inaueleza upingamizi kuwa jambo la kuzuia tukio fulani lisitendeke, kikwazo, kizuizi. Mfano, ningeenda. Awali tulikuwa tumeeleza kuwa mhusika mkuu Katango analiongoza kundi la vijana katika kuutwaa uongozi wa Pango kutoka kwa kikundi cha wazee wanaoongozwa na mhusika Ngwese. Katango akishirikiana na kundi la vijana kama vile Kibwana na Kikubi anafanya kila jitihanda ili kuutwaa uongozi na kuleta mageuzi.

Katika mchakato huu wote, anakumbana na pingamizi nyingi kutoka kwa wazee kama Ngwese,Ngoi, Malebo, Seki na Kauleni. Aidha Mbabekazi ambaye ni mwanamke mwenzake anakuwa kikwazo kwake Katango. Licha ya pingamizi hizi zote anafaulu katika kuutwaa uongozi na kuleta mabadiliko katika Pango.

### 3.2.2 NGWESE: MWAKILISHI WA UTAMADUNI KANDAMIZI

Ngwese- Mwanamume wa makamo ndiye kiongozi wa Pango. Ni mfisadi na mwenye ubinafsi mwingi na anayeendeleza ufisadi mwingi kwa mfano anapowakuta Susa na Sota wakichota maji kisimani anawafukuza. Jambo hili linamkera Katango kiasi kwamba anakabiliana na Ngwese bila kujali tabaka lake katika jamii kwa kusema

> Je, unadhani ubabe wako
> unanitisha mimi? Mimi sio
> hawa watoto unaowafukuza
> watakapo kuchota maji (uk 10)

Ngwese anamdunisha Katango kutokana na jinsia yake ya kike na anatumia ubabe-dume kama kisingizio kuwa, Katango hawezi kupewa nafasi na jamii ya Pango ili aongoze.

Tunaona kuwa Jamii ya Pango inaongozwa kwa mfumo wa ubabe-dume na ndiposa Ngwese anasema kuwa mwanamke hawezi kamwe kumtisha.

Momamyi (1998), anaeleza kuwa mifumo ya kuumeni ni utaratibu mrefu wa masharti ambao unachukuliwa kumaanisha kule kuhalalishwa kwa asasi za kijamii zenye kuhimili tofauti za kiuana katika ugawaji wa kazi. Huu ni mfumo ambao unampa mwanamume nguvu dhidi ya mwanamke katika nyanja zote za kimaisha. Katika ugawaji wa majukumu chini ya mfumo huu, wanawake wanapewa nafasi ya pili baada ya

wanaume. Ngwese anaamini kuwa kumzaba Katango makofi na hatimaye kuolewa, kutamfanya atiwe adabu na mumewe na hatimaye iwe ni kizuizi cha kuudhihirisha ujagina wake kwa kusema,

*Nitakupapata makofi wewe.*

*Naona unanikosea adabu!*

*Unatakiwa kuolewa, utiwe*

*adabu na mumeo!* (uk 14)

Licha ya vitisho vinavyotolewa na Ngwese dhidi ya katango, Katango ameivunja mikatale yote ya utamaduni kutokana na elimu yake na yuko radhi kuyaleta mabadiliko katika Pango.

### 3.2.3 BABAKE KATANGO: ISHARA YA UPINZANI DHIDI YA UJAGINA WA MWANAMKE.

Seki- baba yake Katango, Sota na Susa ni kikwazo kikubwa kwa Katango kwenye harakati zake za kuleta ukombozi kwa wanapango. Yeye (Seki) tungetarajia amuunge mkono bintiye katango lakini kinyume na haya anamuunga mkono Ngwese katika kuendeleza ubinafsi na ufisadi katika nchi ya Pango.

Lugano (1989), anasema kwamba mfumo wa Jamii kongwe umemsaidia mwanamume kujenga fikira kuwa yeye ni bora kuliko mwanamke na kwamba mwanamke lazima ajidunishe mbele ya mwanamume.

Katika uk wa (16 – 17) Susa na Sota wanapokuwa wakimsimulia mama yao ukatili wa Ngwese kwa kuwakataza maji, Katango anaingia nyumbani akiwa ameshika uta na

upote . Anaposikia kuhusu kukatazwa maji kwa watoto anafoka na kushangaa ikiwa ni kweli Ngwese ndiye angefanywa mlinzi wa Pango:

Wakati huo Seki anaingia na kusimama mlangoni anapoambiwa kuwa Ngwese aliwakataza watoto kuchota maji kisimani anadai kuwa huo ulikuwa uzushi na uongo tu ! Katango anaingilia na kusema kuwa huo si uongo. Ubishi baina ya Katango na Seki (Baba yake) unazuka.(uk 17)

Seki babake Katango anadhihirisha kuathiriwa na tamaduni kandamizi dhidi ya mwanamke. Anamkaripia Katango eti ameshika mata na mishale mkononi. Kulingana na Yeye ni Mwanamume tu anayestahili kushika zana hizo. Seki anadai kuwa elimu ya kizungu aliyoipata katango ndiyo inayompa ujasiri wa kupuuza mila. Tunaona kuwa Jamii ya Pango inaongozwa na ubabe-dume na ndiyo sababu ya kusingizia elimu ya kizungu kama pingamizi ya mila kandamizi (uk 18)

Bell na Offen (1977), wanasema kuwa mwanamke hapaswi kupewa elimu sawa na mwanamume. Mwanamume anapaswa kupewa elimu ya juu zaidi ili kupata ujuzi wa kutekeleza majukumu mazito aliyopewa na wanajamii.

Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika inatambua kwamba mwanamke wa Kiafrika anaweza kujikomboa na kuishi vyema bila unyanyasaji huu . Katango amesoma , na mwono ulimwengu wake ni sambamba na ule wa Ufeministi wa Kiafrika.

Seki amesimama kidete kumpinga Katango asipiganie uongozi wa Pango. Katango kwa upande wake haelekei kuliachilia mbali azimio lake. Anadai kuwa ana haki ya kuania uongozi kama Mwanapango yeyote Yule.(uk 20)

### 3.2.4 MBABEKAZI KAMA MWAKILISHI WA MFUMO WA KI-UBABEDUME

Mbabekazi ni msichana; rafiki yake Kikubi. Japokuwa ni rafiki yake Katango, hana imani kwamba Katango anaweza kuchaguliwa kuliongoza Pango. Inaonekana amesongwa sana na utamaduni wa jadi unaogawa majukumu kwa misingi ya kijinsia . Haamini kuwa Wanapango wanaweza kumchagua Katango kuwa kiongozi wa Pango (uk 25)

Mbabekazi wanapokutana na wenzake katika hoteli anaonelea kwamba katango hawezi kuingoza Pango eti kwa sababu yeye ni mwanamke. Anasema kuwa utamaduni wa wanapango hauwezi kumruhusu mwanamke awaongoze. Licha ya kuwa anashawishiwa na Kibwana na Kikubi kuwa Katango ana nafasi ya kushinda na kuwa kiongozi wa Pango, mtazamo wake ni tofauti kabisa. Anaidunisha jinsia ya kike katika suala la uongozi kwa kusema,

> *Haiwezekani! Culture, culture*
>
> *bwana, unafikiria watu watakubali*
>
> *mwanamke awaongoze wewe?*
>
> *We are not yet there*!(uk 25)

Baada ya kauli inayotolewa na Mbabekazi akiuhoji uwezo wa mwanamke katika uongozi Katango anamsuta Mbabekazi na kumwambia kuwa mwanamke ni Mwanapango na ana uwezo wa kufanya mambo mengi ikiwa ni pamoja na uongozi. Muhimu ni ushirikiano na kutojidharau (uk 27)

Wafula na Njogu (2007), wanasema kuwa watetezi wa Ufeministi wa Kiafrika wanaamini kuwa udunishwaji wa mwanamke ulitokana na mila na itikadi za Kiafrika .

Mila na itikadi hizi hugawa majukumu ya mwanamume na mwanamke katika Jamii na kwamba majukumu haya humpendelea mwanamume kuliko mwanamke kwa hivyo, Ufeministi wa Kiafrika hupania katika kumpa mwanamke uhuru dhidi ya asasi kandamizi zinazoongozwa na ubabe- dume na matokeo yake yawe ni kumpa mwanamke ushirikishwaji usiodhibitiwa katika nyanja zote za kijamii. Kwa ufupi Wafula na Njogu wanasema Kwamba watetezi wa Ufeministi wa Kiafrika wana lengo la kudhihirisha juhudi zilizoanzishwa na mwanamke wa Kiafrika za kutathmini na kudai nafasi yake katika Jamii ya Kiafrika.

**3.3 HITIMISHO**

Katika sura hii, tumelishughulikia dhihirisho la ujagina wa Katango miongoni mwa wazee. Tumeeleza kuwa kundi hili linaongozwa na Ngwese, Seki na Ngoi miongoni mwa wengine. Hawataki kuachia vijana uongozi. Vilevile tumeangalia dhihirisho la ujagina wa katango miongoni mwa vijana. Tumesema kuwa kikundi hiki kinaongozwa na Kibwana, Kikubi Mbabekazi na Wengine. Kikundi hiki mbali na Mbabekazi , wanapania kumshika, Kumwongoza na Kumuunga mkono Katango katika harakati za kugombania uongozi wa Pango. Hatimaye vijana hawa wanafaulu na kumtimua Ngwese kutoka uongozini.

Mwisho katika sura hii, tumezichambua pingamizi zinazomkabili katango katika kudhihirisha ujagina wake. Pingamizi ya Kwanza tukasema ni mzee Ngwese. Anapigana kwa jino na ukucha asalie katika uongozi licha ya uroho, ubinafsi na ufisasdi anaouendeleleza. Tumeeleza kuwa Seki babake Katango, ni kikwazo kikuu. Utamaduni kandamizi umemtamalaki na anaamini kuwa Katango hafaai kumpinga Ngwese kwa

vigeso vya kijinsia. Anaudara uwezo alionao katango katika kuiongoza Pango. Pingamizi nyingine imetokana na Mbabekazi. Huyu licha ya kuwa ni mwanamke ambaye anatarajiwa kuupinga mfumo wa ki-ubabedume anauunga mkono kwa kudai kuwa, kwa vile Katango ni mwanamke utamaduni haumruhusu kuwania uongozi katika Pango.

# SURA YA NNE

# WAHUSIKA WENGINE WANAVYOCHANGIA UJAGINA WA MWANAMKE KATIKA *PANGO*

## 4.0 UTANGULIZI

Katika sura hii, tutaonyesha jinsi wahusika wengine (wa kike na wa kiume), wanavyochangia katika kuudhihirisha ujagina wa mwanamke katika *Pango.* Wahusika wa kiume tuliowaangazia ni pamoja na Kibwana; mwanamume Kijana; rafiki yake Katongo, Kikubi; mwanamume kijana, Babu; Mzee; babake Ngwese, Sota; Mvulana wa miaka kumi na mmoja; ndugu yake Katango na Susa.

Kwa upande wa wahusika wa kike, tumewaangazia wahusika wafuatao: Mama – mamake Katango; Susa na Sota, Sakina – mkewe Ngwese, Susa – msichana wa miaka kumi; ndugu yake Katango na Sota.

## 4.1. WAHUSIKA WA KIUME WAVYOCHANGIA KATIKA KUUDHIHIRISHA UJAGINA WA MWANAMKE KATIKA *PANGO.*

Jamii ya Pango inaonekana kutawaliwa na mfumo wa ki-ubabedume kama inavyodhihirishwa na wahusika Ngwese, Ngoi na Malebo. Lakini hata hivyo, kuna wahusika wa kiume ambao wanapania kuupinga ubabe–dume huu na kuuzika kwenye kaburi la sahau kwa kumuunga mkono Katango katika harakati zake za kutafuta uongozi wa Pango.

Abbenyi (1997) anasema kuwa lengo la Ufeministi wa Kiafrika ni kujenga jamii inayothamini usawa wa kijinsia na kwamba ufeministi huu ni muhimu sana kijamii,

kiuchumi, kiutamaduni na katika nyanja zote za maisha ya kila siku. Njogu na Wafula (2007) wanasema kuwa watetezi wa Ufeministi wa Kiafrika wanaamini kuwa udunishwaji wa mwanamke ulitokana na mila na itikadi za Kiafrika. Mila na itikadi hizi hugawa majukumu ya mwanamume na mwanamke katika jamii na kwamba majukumu haya humpendelea mwanamume kuliko mwanamke. Kwa hivyo, Ufeministi wa Kiafrika hupania kumpa mwanamke uhuru dhidi ya asasi kandamizi zinazoongozwa na ubabe-dume na matokeo yake yawe ni kumpa mwanamke ushirikishwaji usiodhibitiwa katika nyanja zote za kijamii. Wanaendelea kusema kwamba watetezi wa Ufeministi wa Kiafrika wana lengo la kudhihirisha juhudi zilizoanzishwa na mwanamke wa Kiafrika za kutathmini na kudai nafasi yake katika jamii inayoongozwa na ubabe-dume.

### 4.1.1 KIBWANA KAMA MSHIRIKI KATIKA KUUDHIRISHA UJAGINA WA KATANGO

Mazungumzo baina ya Kibwana na wenzake hotelini yanaonyesha bayana kwamba, anamuunga mkono Katango katika dhamira yake ya kutwaa uongozi. Anapotaniwa na Kikubi kwa kumwuliza gazeti linasema ulimwengu ungeisha lini, Kibwana haonekani kuudhika bali anawafafanulia kuhusu nia ya Katango kuwaania uongozi. Ni dhahiri kuwa, Kibwana licha ya kuwa miongoni mwa jamii inayotawaliwa na mfumo wa ki-ubabedume, mtazamo wake kuhusu jinsia ya kike ni chanya. Anaendelea kumpinga Mbabekazi kwa dhati anapodai kuwa Katango hangeweza kuchaghuliwa na Wanapango (uk 25).

Kibwana anamuunga mkono Katango kwa dhati katika harakati zake za kutafuta uongozi. Kibwana anajidhihirisha kama mtetezi wa mwanamke dhidi ya mfumo wa kiubabe-dume

ambao umemkandamiza mwanamke wa Kiafrika. Kulingana na Mbatiah (2000:87) nadharia ya ufeministi inajishughulisha na utetezi wa haki za wanawake dhidi ya ukandamizwaji katika jamii zenye mifumo iliyodhibitiwa na wanaume. Birke (1986) na Lovenduski na Randall (1993) wanadai kwamba, ufeministi ni dhana inayoelezea hali ya wanawake kujieleza katika jamii, mbali na wanaume wanaounga mkono jitihada za wanawake hao.

Kutokana na mazungumunzo kati ya Kibwana na Katango, ni dhahiri kuwa Kibwana ana imani kuwa Katango angeshinda na ndipoas anamhakikishia kuwa hali ni nzuri na pia matumaini yapo (uk 31) Kibwana haonekani kujitenga na Katango katika dhiki na raha za kuwania uongozi wa Pango kama inavyodhihirika katika ukurasa wa 33.

Kwenye uwanja wa mikutatno karibu na Pango Kibwana anaendelea kumuunga mkono Katango kwa kuliongoza kundi la vijana kumfanyia katango kampeni, vijana hawa wanayapiga magoma makubwa makubwa na kupiga vigelegele vingi kama ishara ya kumwuunga mkono Katango. Kibwana anawaongoza kwa kuimba na kukariri kwamba,

*Upepo umebadili majira, haya*
*ni mengine majira kale iliyokuwako*
*imechwewa na jua la ufahamu*
*limetuchea, vijana!! Hatutishwi*
*na kupigwa Kabari ii !* (uk 36)

Kulingana na Millet (1977) Ufeministi wa Kiafrika uliibuka ili kuwahusisha wanawake katika mawanda mapana ya shughuli za kijamii miongoni mwa jamii za Kiafrika. Kwa hivyo ufeministi huu husisitiza ugawanaji sawa wa majukumu ya kijamii miongoni mwa

wanaume na wanawake. Kibwana ni mtetezi shupavu wa haki za wanawake. Licha ya kuwa Katanga ni rafiki yake, anaonekana kuupinga mfumo wa ubabe-dume katika jamii. Hachoki kumpigia Katango debe miongoni mwa vijana wenzake. Katika mkutano uliofanyika uwanjani, Babu anapofaulu katika kuutuliza umma, Kibwana anasema,

> *Katango nishujaa. Anawaongoza vijana*
> *wenzake kumwinua na kumbeba juu*
> *kwa juu kwa muda (uk 47)*

Katika uwanja wa mkutano, Ngwese anapofaulu kuwavuta Wanapango wengi upande wake kwa kuwahongo na matunda, Kibwana akiwa na Kikubi, Susa, Sota, Mama, wanawake wawili watatu na vijana wachache wanasimama kidete na kubaki upande wa Katango. Baada ya tukio hilo, Kibwana na Kikubi walienda kwa akina Katango kumliwaza. Hawa wawili, wanaungama kuwa wanauhisi uchungu kama vile Katango alivyouhisi alipotelekezwa na Wanapango katika uwanja wa mkutano. (uk. 58) Katika kumuunga mkono Katango, Kibwana anadhihirisha kwamba, yeye ni mtetezi shujaa wa haki za mwanamke na anapinga mfumo wa ki-ubabedume.

Mrengo wa ufeministi huru unaunga mkono kauli hii kwani hutetea usawa kati ya wanawake na wanaume katika ngazi zote za maisha. Mrengo huu hushikilia kwamba, maadamu wanadamu wameumbwa kuwa viumbe sawa, wote wanawake kwa wanaume wanapaswa kuwa huru kutekeleza majukumu na malengo yao maishani.

### 4.1.2 KIKUBI: ISHARA YA KUJITOLEA KWA VIJANA KUUDHIHIRISHA UJAGINA WA MWANAMKE.

Kikubi ni mhusika anayechangia udhihirika wa ushujaa wa mwanamke katika *Pango.* Anaungana na vijana wenzake katika kupigania haki za mwanamke. Anataka Katango awe kiongozi wa Pango. Amekiuka mtazamo wa kiutamaduni katika jamii ya Wanapango kuwa mwanamke hapaswi kuongeza jamii. Yeye anaupinga mfumo wa kiubabe-dume hasa miongoni mwa jamii za Kiafrika. Anaamini kuwa mwanamke hapaswi kufungwa kwa pingu za tamaduni na kwamba mwanamke akipewa nafasi sawa na mwanamume anaweza kuudhihirisha ujagina wake barabara katika nyanja zote za kimaisha. Kikubi anaungama kwamba Katango ni jagina na anaweza akaongoza pango bila tashwishi yoyote. Anamsifu sana kwa kusema walisoma naye na kwamba hata wanaume walikuwa wakimwogopa.

Kikubi walipokutana na wenzake na kuambiwa na Kibwana kuwa Katango alikuwa akinuia kujitoma uwanjani mwa siasa na kupambana na Ngwese katika kuutafuta uongozi. Mbabekazi alipouhoji uwezo wa Katango wa kuiongoza Pango kwa kigezo cha jinsia yake, Kikubi aliutetea uwezo wa Katango kwa kusema,

> *Ahh huyo? Nimesoma naye…*
> *aliwahenyesha wanaume ile*
> *mbaya kutokana na misimamo yake.*
> *Ana ujasiri sana beibei Yule* (uk.25).

Mbabekazi ambaye ni rafiki yake Kikubi haonekani kashawishika kwamba Katango anaweza kuwa kiongozi wa Pango. Yeye ni mwanamke ambaye badala ya kumuunga mkono Katango, ili wajikwamue kutoka pingu za ubabe-dume, anaonekana kuunga

mkono mfumo kandamizi wa ubabe-dume. Kikubi anashangazwa na mtazamo huu wa rafiki yake na ndipo akamwambia Kibwana kuwa, adui wa mwanamke ni mwanamke mwenyewe. (uk. 25)

Kikubi anaendelea kumuunga mkono Katango anaposema kwamba japokuwa kondoo hana pembe anaweza kukivunja chungu. Usemi huu unaonyesha kuwa Kikubi ni mtu ambaye ana upeo wa mbali na wala hajafungwa na tamaduni kandamizi zinazomnyanyasa mwanamke wa Kiafrika. Ni dhahiri kuwa baadhi ya wanawake wa Kiafrika ni wachangizi wa ukandamizwaji wa wanawake wenzao na jamii yenye mfumo wa ki-ubabedume. Wanawake kama hawa huamini kuwa, mwanamke hana nafasi ya kuudhihirisha ujagina wake na kwamba, uongozi thabiti na ulio bora hutokana na wanaume. Millet (1977) anaunga mkono kauli hii kwa kusema kuwa, Ufeministi wa Kiafrika uliibuka ili kuwahusisha wanawake katika mawanda mapana ya shughuli za kijamii miongoni mwa jamii za Kiafrika.

Wafula na Njogu (2007:50) wanuanga mkono kauli hii kwa kusema kuwa msingi wa Ufeministi ni kupigania ukombozi wa mwanamke kutokana na pingu za kiutamaduni, kidini, kijamii, kisiasa na kiuchumi. Kikubi anaendelea kumtetea Katango wanapokuwa kwenye uwanja wa mkutano. Anamlinganisha Katango na jiwe la mango ambalo huvunja mauongo. Ngwese alipokuwa akihutubia hadhira katika uwanja wa mkutano na kudai kwamba fahali mzee hupigana kwa ustadi, Kikubi anamkata kauli na kumwambia kuwa, kitu kizuri kizeekapo ni tumbako. (uk 46)

### 4.1.3 BABU: KIWAKILISHI CHA UMOJA WA KIZAZI KIPYA NA KIZAZI CHA KALE

Babu (babake Ngwese) japo ni mzee wa kizazi cha kale anakwenda kinyume na matarajio anapomuunga mkono Katango kuliongoza Pango. Pia tungetarajia amuunge mkono mwanawe Ngwese. Amekombolea kutokana na utamaduni wa Wanapango ambao haumthamini mwanamke hasa kwenye masuala ya uongozi. Mbatiah (2000:87) anasema kuwa Ufeministi ni nadharia ya kifasihi ambayo inajishughulisha na utetezi wa haki za wanawake dhidi ya ukandamizwaji katika jamii yenye mfumo uliodhibitiwa na wanaume. Birke (1986) na Lovenduski (1993) wanadai kwamba, Ufeministi ni dhana inayoelezea hali ya wanawake kujieleza katika jamii, mbali na wanaume wanaounga mkono jitihada za wanawake hao.

Babu ndiye anayeiongoza hadhira kwenye uwanja wa mkutano. Katika maongezi yake ya ufunguzi baada ya kutuuliza umati, ni wazi kwamba yeye anauunga mkono kizazi cha vijana. Hii inadhihirika anapowahutubia Wanapango kwa kutumia misemo na kusema kuwa, kuku aliyewahi kupapurwa na kipungu hujanjaruka na pia anaongeza kwamba, maua yamechanua na karibu nyuki watarudi pangoni na kuanza kutengeneza asali. Vilevile anawashauli Wanapango hasa vijana kuwa, sharti waitetee asali. Bab kwa kutumia misemo hii ana maana kwamba, ana matumaini makubwa kuwa Katango atamshinda Ngwese na kuutwaa uongozi. (uk 40)

Babu katika hotuba yake anaonyesha waziwazi kuwa amechoshwa na uongozi wa mwanawe Ngwese. Anamfananisha Ngwese na ndeme na wishwa. Anamtambua Mwanawe kuwa ni mwongo. Hivyo basi, anawashauri Wanapango wamchangue

kiongozi asiyekuwa mwongo wa kuungaunga uongo.Babu amemtambua Katango kama jagina wa Wanapango na ndiposa anamtembelea nyumbani kwao na kumliwaza kutokana na hali ilivyokuwa kule uwanjani. Anampongeza kwa kujikaza kisabuni licha ya Wanapango wengi kwenda upande wa Ngwese baada ya kuhongwa kwa matunda. Anamhimiza aendelee na jitihada zake za kuutafuta uongozi wa Pango na asikate tamaa (uk 40)

Babu ni muungaji mkono wa Ufeministi wa Kiafrika na anaelewa kwamba, mwanamke ana uwezo sawa na mwanamume katika nyanja zote za maisha. Hii inadhihirika anapoungama mbele ya Katango kuwa, yeye (Katango) ndiye aliyekuwa ameshinda lakini aliponywa ushindi na akina Ngwese kama fisi wanavyoing'wafua nyama iliyo kinywani mwa simba. (uk 57). Katango anapoelekea kukata tamaa ya kuupigania uongozi wa Pango kwa kutatizwa na kizazi cha kale kikiongozwa na Ngwese, Babu anamtia shime kwa kumwambia kuwa, mwewe anapochukua kuku, si halali kumrushia mayai. Aidha Babu anamshauri kuwa uchungu wa uzazi hauwazuii wanawake kushika mimba. Hatimaye, Kibwan na Kikubi wanapojiunga nao, Babu anawashauri wasikate tamaa katika harakati zao za kuutafuta uongozi. (uk 58)

Babu anaungama kwamba, vijana ndio tegemeo la jamii ya Wanapango na kuwa mtoto ni mguu wa tatu wa mzazi na sharti wazazi wawahimize hata hali inapokuwa ngumu.(uk.60) Kwenye mazungumzo baina ya majitu watatu, Katango analipovuta vazi la mmoja wa majitu, Babu anashtuka sana anapogundua kwamba huyo alikuwa Ngwese. Anashangaa na kutoa kauli kuwa, mvunja Pango ni mwanakijiji kwa maana kuwa Ngwese ndiye mvunja Pango. (uk 86)

Kutokana na maongezi ya Babu, inadhihirika kuwa yeye ni mzalendo wa Pango. Kamwe hamuungi mkono Ngwese katika kuendeleza ufisadi licha ya kuwa Ngwese ni mwanawe. Yeye anaamini kwamba, vijana hasa wa kike wakipewa nafasi wanaweza kuudhihirisha ujagina wao katika uongozi.

### 4.1.4 SOTA KAMA MWAKILISHI WA VIJANA KATIKA KUUNGA MKONO UJAGINA WA KATANGO.

Sota ni mvulana wa miaka kumi na mmoja; ndugu yake Katango na Susa. Licha ya umri wake mdogo, haogopi kumpigania na kumuunga mkono dadake Katango kwenye harakati za kuutafuta uongozi wa Pango. Kulingana na Steady (1981:30-37) Ufeministi wa Kiafrika unatambua uhusiano wake na Ufeministi wa Kimataifa lakini unafafanua Ufeministi ambao una mahitaji na malengo maalum yanayotokana na uhalisi wa maisha ya wanamke katika jamii za Kiafrika. Ufeministi huu vilevile unaheshimu uwezo wa mwanamke wa Kiafrika wa kujitegemea na kupuuza unyanyaswaji wa utumwa unaomkabili. Unatambua jitihada za mwanamke katika kupigania haki zake katika jamii ambazo zimekuwa na vita vya ukombozi wa kitaifa na ujenzi mpya wa jamii zenye usawa wa kijinsia.

Sota na Susa wanapokutana na Ngwese kisimani na Ngwese anawafukuza, Sota licha ya umri wake mdogo, anabishana na Ngwese na kusimama kidete kutetea haki yake ya kuchota maji. Ngwese kwa ukali mwingi anapowakiripia Sota na Susa na kuwatuhumu kuwa wanaichezea ardhi yake aliyoitolea jasho, Sota anamjibu bila wasiwasi wote kuwa, hawaichezei ardhi bali wanachokitaka ni maji tu. Ngwese anapoendelea kudai kuwa kazi yao ni kucheza, Sota anashikilia kuwa kazi yao si ya kucheza pangoni.(uk 6)

Katango na Kibwana walipovamiwa na Mtu I na Mtu II walipokuwa njiani, Sota ndiye aliyefyatuka kama mshale kwenda kumwita mamake Katango. (uk 33) Katika uwanja wa mkutano,Katango anapoanza kutoa hotuba yake kwa hadhira, Sota na Susa ndio tu wanaoitikia wakati Katango anapoitambaa hadithi.(uk 42)

Katango anapoendelea na hadithi, Sota anaendelea kudakiza kama ishara ya kumuunga mkono dadake Katango kwa kusema kuwa kisima ni cha kutumiwa na wanajamii yote yote ya Wanapango. (uk 43) Sota mbali na kuwa mvulana mwenye umri mdogo anatambua haki zake kama Mwanapango. Vilevile anachangia katika kuuchangia ujagina wa Katango.

### 4.1.5 MAMA KATANGO: ISHARA YA USHIRIKIANO WA WANAWAKE

Mamake Katango, Susa na Sota na mkewe Seki, anajidhihirisha kama mlezi wa jamii thabiti. Amejitolea kumlea na kumsomesha Katango hadi akawa shujaa anayetaka kuwaongoza Wanapango. Malengo ya Katango ni kuumaliza ufisadi katika Pango na kuuleta mwanzo mpya . Mama ameachiwa majukumu yote ya ulezi na mumewe Seki ambaye kazi yake ni kuzurura huku na huko akimuunga mkono Ngwese katika kuendeleza ufisadi na ubabe-dume katika Pango. Mama anamuunga mkono Katango katika juhudi zake za kutafuta uongozi.

Millet (1977) anaeleza kuwa Ufeministi wa Kiafrika uliibuka ili kuwahusisha wanawake katika mawanda mapana ya kijamii miongoni mwa jamii za Kiafrika. Husisitiza ugawanaji sawa wa majukumu ya kijamii miongoni mwa wanaume na wanawake. Mama Anapoambiwa na watoto kuwa kisima cha pili kimezungushwa seng’enge anapinga hali

hiyo ya uroho na ubinafsi na kushangaa ikiwa Ngwese alitaka kukitumia kisima pekee. (uk 16)

Seki anapodai kuwa Sota na Susa wamechochewa na Katango ili wadanganye kuwa wamekatazwa kuchota maji kutoka kisimani na Ngwese, Mama anasimama na mwanawe Katango na kumwambia Seki kuwa Katango anasema ukweli. Seki anaposema watoto wapuuzwe wanaposimulia kadhia zilizowapata pale kisimani, Mama anasimama na wanawe na kusema kuwa haifai kuwapuuza watoto kwa kigezo cha umri wao. (uk 19) Mama ni mlezi mwema na amewafunza wanawe (Sota na Susa) kazi ya kuchunga. Habagui watoto wake kwa misingi ya kijinsia.

Wafula na Njogu (2007) wanasema kuwa, watetezi wa Ufeministi wa Kiafrika wanaamini kuwa udunishwaji wa mwanamke ulitokana na mila na itikadi za Kiafrika. Mila na itikadi hizi hugawa majukumu ya mwanamume na mwanamke katika jamii na kwamba majukumu haya humpendelea mwanamume kuliko mwanamke. Kwa hivyo, Ufeministi wa Kiafrika hupania katika kumpa mwanamke uhuru dhidi ya asasi kandamizi zinazoongozwa na ubabe-dume na matokeo yake yawe ni kumpa mwanamke ushirikishwaji usiodhibitiwa katika nyanja zote za kijamii. Seki anapowahutumu Sota na Susa kuwa wanachezea pangoni, Mama anasimama kidete na kuwatetea dhidi ya tuhuma hizi. Mama anamwambia Seki kuwa, Sota na Susa wanalistahi Pango na kamwe hawawezi kuichezea kwani wameelezewa thamani yake na babu yao .(uk 21)

Seki analiposema kuwa pango limegeuzwa uwanja wa kufanyiwa kila aina ya upuuzi, Katango hakukubaliana na kauli hiyo. Alimpinga babake na kudai kuwa hiyo ilikuwa sababu tosha ya kuteuliwa kiongozi afaaye kuliongoza Pango. Malumbano baina ya

Katango na babake yanapozidi, Mama anaituliza hali kwa kudakia na kusema kwamba, ni bora siku ya kuchaguliwa kwa kiongozi mpya ifike ili wanawe wasilaumiwe tena eti ndio wanaochezea Pango. (Uk 22) Seki anapomzomea Katango kwa kukiuka utamaduni wa jamii ya Pango na kususia kupashwa tohara, mamake Katango anamtetea vikali na kumwambia Seki asiyazungumze hayo mbele ya watoto.(uk 19) Katango na Kibwana walipovamia walipokuwa njiani, Mama ndiye aliyekuwa wa kwanza kuja kuwaokoa na kuwapa pole.(uk 33)

Mama anaendelea kumsitikitikia Katango kwa kumshauri aache kugombea uongozi kwa sababu Ngwese yuko radhi hata kumwangamiza. Katango anajipa moyo na kumwambia mamaye kuwa ataendelea kuwania uongozi na mwishoni watu watajua ubaya wa Ngwese.

Mamake Katango ameachiwa majukumu yote ya malezi lakini hata hivyo hafi moyo. Yeye ni mama anayejali watoto wake licha ya kuachiwa majukumu haya na mumewe. Mama ndiye anayetuchorea taswira ya jinsi mwanamke anavyokandamizwa na mwanamume kupitia wimbo wake. Anadai kuwa, Seki (mumewe) amegeuka umande jua lipigapo na kuwa ameisusia kazi. Vilevile mama anasema kuwa, Seki amekuwa mwenye lawama na kisha anadai chakula kwa fujo. Mama anazidi kulalamikia hali ya wanawake kwa kusema,

*wake tumedhalilika na kuteseka.*
*Kuni kutafutana watoto*
*juu migongoni chakula kutafuta*
*na kuandaajikoni huko wenzetu*

*njiani wanazishikakwenda kuzama*

*kwenye karamu…* (uk 55-56)

Katika mkutano uliofanyika uwanjani, Nagwese akawahonga watu kwa matunda, na wakaacha Katango peke yake, Mama alisimama naye katika hali hiyo ya upweke.

Maelezo haya yote kumhusu Mama yanaonyesha kujitolea kwake kama mama mlezi wa Katango na mwelekezi mwema. Anamuunga mkono Katango katika kutafuta uongozi wa Pango. Yeye pia ni mama mwenye huruma na asiyewabagua watoto wake kwa misingi ya kijinsia. Anauendeleza ujagina wa mwanamke katika *Pango.*

**4.1.6 SAKINA: ISHARA YA MUUNGANO WA WANAWAKE**

Sakina ni mkewe Ngwese, ni mwanamke wa umri wa makamo. Ni mwanamke mwenye utu na anajidhihirisha kama mtetezi wa wanyonge licha ya kuwa mkewe Ngwese ambaye anauendeleza ufisadi na ubinafsi katika Pango. Yuko radhi kukosana na mumewe kwa kutetea haki za wanyonge. Ni mtu mwenye huruma na anayeukosoa uongozi wa Ngwese japokuwa ni mumewe. Sota na Susa walipokatazwa kuchota maji, alilalamikia tukio hilo na kumkashifu mumewe Ngwese kwa kutokuwa na utu na huruma. Sakina anaposikia mumewe Ngwese akiwagombeza akina Sota na Susa anataka kujua kinachoendelea. Ngwese anapomwelezea sababu za ghasia na kelele, Sakina anamzomea mumewe bila kujali na kumwambia kuwa, ni makosa kuwakataza watoto maji kwani hata kama ardhi ni yake, watoto hawaichukui bali haja yao ni maji. Anamkumbusha Ngwese kuwa, watu huishi kwa udugu.(uk 7) Sakina ni mwanamke aliyekomaa kimawazo na mwenye mwono ulimwengu mpevu akilinganishwa na mumewe Ngwese, Anauthamini udugu na ushirikiano wa Wanapango na pia ni mwenye hekima.

Anaukashifu ubepari huku akiuthamini ujamaa. Haoni haja yoyote ya mumewe kuwakataza wanajamii wachote maji kutoka kisimani. Nyumbani kwa Ngwese, Sakina anapogundua kuwa mumewe haendi kazini, anamkumbusha ahadi alizowatolea Wanapango kabla ya kuchaguliwa. Anamrai kuhusu wajibu wake kwa Wanapango na kumweleza kuwa, Pango linatazamwa na wengi kinyume na mambo yalivyokuwa hapo awali alipokuwa anafanya kazi katika shirika. Kwa kutumia msemo, Sakina anamwambia Ngwese kuwa, siku moja panya watawazia kumvika paka kengele (uk 50-51) Sakina ni mwanamke anayetetea haki za Wanapango na yuko radhi kumzomea mumewe Ngwese anapogundua kwamba ameupuuza wajibu wake kwa Wanapango. Ni katika mazungumzo yake na Ngwese tunapouona ufisadi ulioendelezwa na Ngwese alipokuwa akifanya kazi kwenye shirika fulani. Sakina ameudhihirisha ujagina wa mwanamke miongoni mwa Wanapango.

### 4.1.7 SUSA KAMA ISHARA YA MWAMKO MPYA WA WANAWAKE

Susa ni msichana wa umri miaka kumi na ndugu yake Katango na Sota. Licha ya umri wake mdogo, ameudhihirisha ujagina wake kama mtoto wa kike asiyeogopa. Anafahamu haki zake na yuko tayari kujitetea katika hali zote.Kisimani yeye na Sota wanapofukuzwa na Ngwese, anasimama kidete na kubishana vilivyo. Anashirikiana na nduguye Sota kwenda malishoni licha ya kuwa kazi ya kuwapeleka mifugo malishoni huchukuliwa na wanajamii kuwa ya wavulana. Allan (1995) anazihoji asasi za kijamii ambazo zimemkweza mwanamume na kumdunisha mwanamke. Anaendelea kusema kuwa Ufeministi wa Kiafrika huhoji asasi za kijamii ambazo huzuia mwanamke wa Kiafrika kujitambua na kujiamini. Kiini hasa cha kupigania usawa baina ya mwanamume na mwanamke ni kutafuta sauti ya kike, uhuru wa mawazo na vitendo. Pia kumhusisha na

kumpa nguvu mwanamke katika maisha ya kila siku. Ngwese anapowakuta Sota na Susa kisimani na kudai kuwa kazi yao ni kucheza Susa anakataa katakata na kumwambia Ngwese kuwa, kamwe hawakuwa wakilichezea Pango. (uk 6) Mbele ya babake (Seki) Susa anaendelea kujitetea kwa ujasiri mwingi babake anapomtuhumu kuwa ndio wanaocheza pangoni. Dadake Katango anaposhambuliwa akiwa na Kibwana, Susa anaonyesha ujasiri wake kwa kukabiliana na wavamizi hao na hata kuwapiga kwa mayai. Anamsimulia babake alivyompiga mmoja wa wavamizi hao kwa yai (uk 35) Katika uwanja wa mkutano, Katango anapoanza kuwahutubia wanapango Sota na Susa ndio wanaoitikia wakati Katango anapoanza kuitambaa hadithi yake.(uk 42). Susa anamuunga mkono Katango katika harakati zake za kuwania uongozi katika Pango. Ana mapenzi ya dhati kwa dadake.

## 4.2 HITIMISHO

Katika sura hii, tumeonyesha jinsi wahusika wa kike na wa kiume wanavyochangia katika kuudhihirisha ujagina wa mwanamke katika *Pango*. Kwenye tapo la wahusika wa kiume, tumewaangazia Kibwana, Kikubi, Babu na Sota. Tumeona kuwa Kibwana anamuunga mkono Katango kwa dhati katika harakati zake za kuutafuta uongozi. Aidha Kibwana ni mtetezi wa mwanawake dhidi ya mfumo wa kiubabe-dume. Kikubi naye anaungana na vijana wenzake katika kupigania haki za mwanamke. Anataka Katango awe kiongozi wa Pango. Amekiuka mtazamo wa kiutamaduni katika jamii ya Wanapango ambao unadai kuwa mwanamke hapaswi kuongoza jamii yenye mfumo wa ubabe-dume. Naye Babu ambaye ni babake Ngwese, anamuunga mkono Katango kuliongoza Pango. Amekombolewa kutoka kwenye utamaduni wa Wanapango ambao haumthamini

mwanamke hasa kwenye masuala ya uongozi. Babu ana imani na uongozi wa vijana licha ya kwamba yeye ni wa kizazi cha kale. Anaamini kwamba vijana wakipewa nafasi wanaweza kuudhihirisha ujagina wao katika uongozi. Mwisho kwenye tapo hili tumemwagazia Sota. Tumesema kuwa, licha ya umri wake mdogo, haogopi katika juhudi zake za kumpigania dadake Katango. Yeye anazitambua haki zake kama mwanapango.

Kwa upande wa wahusika wa kike, tumesema kuwa mamake Katango amejitolea kumlea na kumsomesha Katango hadi akawa shujaa anayetaka kuwaongoza wanapango. Ameachiwa majukumu yote ya ulezi na mumewe Seki lakini haonekani kukata tamaa. Pia ni mama mwenye huruma kwa wanawe. Mhusika mwengine ambaye tumemwangazia ni Sakina ambaye ni mkewe Ngwese. Tumesema kuwa ni mwanamke mwenye utu na amedhihirisha umoja wa wanawake na asiyependa ufisadi na ubinafsi. Mwisho katika tapo hili la wahusika wa kike tumemwangazia Susa. Huyu ni dada mdogo wa Katango. Tumesema kuwa licha ya kuwa yeye ni msichana mdogo, haogopi na anafahamu haki zake na yuko tayari kujitetea katika hali zote. Yeye ni ishara ya mwamko mpya wa wanawake katika jamii hii inayotawaliwa na utamaduni unaombagua mwanamke kwa ushirkikiano na mfumo dhalilishi wa ki-ubabedume.

# SURA YA TANO

# HITIMISHO

## 5.0 UTANGULIZI

Sura hii inashughulikia matokeo ya utafiti wetu kulingana na madhumuni tuliyoyaorodhesha na yale yaliyodhirika katika uchangunuzi wa *Pango*. Aidha tumeyatoa mapendekezo yetu kulingana na mada yetu, tukatoa rai za tafiti za baadaye na hatimaye tumetoa orodha ya marejeleo muhimu kuhusu mada ambayo tumeishughulikia.

## 5.1 MUHTASARI WA MATOKEO YA UTAFITI

Katika utafiti huu, imebainika kuwa Wamitila K.W. amefaulu pakubwa katika kuusawiri ujagina wa mwanamke katika *Pango.* Nadharia tuliyoitumia ni ya Ufeministi wa Kiafrika ambayo imetamalaki katika sura zote tulizozishughulikia. Katika sura ya kwanza tumeonyesha baadhi ya asasi za jamii ambazo ni kikwazo kikuu katika kuudhihirisha ujagina wa mwanamke. Asasi hizi tukasema ni dini, ndoa na asasi za elimu. Aidha imejitokeza kuwa,kuna matapo mbalimbali ya ujagina. Mathalani jagina chanya , jagina hasi, jagina kinzani. Katika utafiti huu tumejikita kwenye tapo la jagina chanya. Jagina wa aina hii huhusishwa na kazi zilizoandikwa katika misingi ya uhalisia wa kisoshalisti. Wahusika wa aina hii wanapaswa kuwa vielelezo kwa jamii na wanaoweza kuitia hamasa ya kushiriki katika mapinduzi ya kuboresha hali yao. Katika sura ya tatu, imejitokeza kwamba Katango ni jagina halisi ambaye amejidhihirisha kama shujaa miongoni mwa wazee na vijana.

Aidha Katango amekabiliana na changamoto za kila aina katika harakati zake za kuudhihirisha ujagina wake na hatimaye ameibuka na ushindi. Wazee wakiongozwa na

Ngwese wamesimama kidete na kumwekea kizingiti kikuu ili asiliongoze Pango. Licha ya haya yote imedhihirika kuwa, Katango ni shupavu na ana ari kubwa ya kuliongoza Pango. Imeibuka kuwa Katango anathaminiwa sana na vijana ambao wako radhi kumuunga mkono ili awaongoze kama kijana mwenzao. Anayewaongoza vijana hawa ni Kibwana, ambaye ni rafiki yake Katango. Vijana hawa wanamuenzi Katango kwa ujagina wake na wako tayari kumpigania kwa jino na ukucha.

Aidha katika sura hii imeibuka kuwa kuna vikwazo vya kila aina ambazo zinamzuia Katango kuudhihirisha ujagina wake. Ngwese ambaye ana uroho na ubinafsi mwingi na anayeendeleza ufisadi wa hali ya juu hataki Katango awe kiongozi wa Pango. Anaamini kuwa mwanamke hawezi kuwa kiongozi hasa miongoni mwa jamii zinazodhibitiwa na mfumo wa ki-ubabedume. Ngwese vilevile anauendeleza utamaduni kandamizi dhidi ya mwanamke. Katika utafiti huu, imedhihirika kuwa baadhi ya wanawake ni vikwazo kwa wanawake wenzao hasa wanapopania kuudhihirisha ujagina wao katika jamii. Mathalani Mbabekazi, anaamini kuwa Katango hawezi kuongoza Pango kwa msingi wa jinsia yake. Anaupinga uongozi wa Katango na kudai kuwa wanajamii hawawezi kumchagua Katango.

Katika sura ya nne, imedhihirika kuwa licha ya vizuizi mbalimbali ambavyo humzuia mwanamke kujidhihirisha kama shujaa miongoni mwa jamii, kuna wanajamii ambao wako radhi kumuunga mkono ili kuafikia lengo hilo. Wahusika hawa ni Kibwana, Kikubi, Susa, Babu, Sota, Sakina na Mama. Katika utafiti wetu, tuliongozwa na nadharia tete kuwa, Wamitila K.W amefaulu pakubwa katika kuusawiri ujagina wa mwanamke katika *Pango.* Hili limedhihirika waziwazi kwa jinsi mwandishi

alivyomsawiri Katango kama jagina licha ya kuzungungwa na jamii inayoongozwa na mfumo wa ki-ubabedume. Aidha katika nadharia tete yetu, tulieleza kuwa kuna changamoto nyingi katika harakati za kuujenga ujagina wa mwanamke katika jamii yenye mfumo wa ki-ubabedume. Mwandishi amefaulu kuzichora changamoto hizi ambazo zinamzingira Katango. Changamoto hizi zinasababishwa na kizazi cha kale kikiongozwa na Ngwese, Seki na Mbabekazi. Hata hivyo Katango amekabiliana nazo na kuibuka jagina katika *Pango.* Kwa hivyo, tumeweza kudhihirisha kuwa nadharia tete zetu ni sahihi.

## 5.2 MAPENDEKEZO

Utafiti huu umedhihirisha kuwa mwandishi wa *Pango,* K.W Wamitila amefaulu pakubwa katika kuusawiri ujagina wa mwanamke. Aidha amedhihirisha kuwa, kuna changamoto nyingi katika harakati za kujenga ujagina wa mwanamke katika jamii yenye utamaduni baguzi na mfumo wa ki-ubabedume. Ili kuibua ujagina wa mwanamke katika jamii zenye mfumo kama huu, tunapendekeza kuwa, watunzi wa kazi za fasihi ya Kiswahili watunge kazi nyingi kwenye tanzu zote za fasihi na kazi hizo ziwe na wahusika wa kike watakaosawiriwa kama majagina ili wawe changamoto muhimu katika kutetea utangamano mzuri wa kijisia katika jamii zetu.

## 5.3 TAFITI ZA BAADAYE

Tunapendekeza kwamba, maadamu tumefanya utafiti wetu kwa kujikita katika *Pango*, tafiti za baadaye zichunguze ujagina wa mwanamke katika tamthilia nyingine. Vilevile kwa vile kwa kuna ugiligili mwingi katika tanzu za fasihi,

wavuke mipaka na wafanyie utafiti mada hii katika tanzu nyingine za fasihi ya Kiswahili.

## MAREJELEO


Adagala K. (1981), " Wanja of Petal of Blood: A Study of the Woman Question and Imperialism in Kenya," Staff seminar paper, University of Nairobi.

Ahmadi, H.A. (1971), *Kurani Tukufu*. (Toleo la Pili) Lahore: Panama Printing Press.

Al-Marzuqui, I.A. (2000), *Human Rights in Islamic Law*. Dubai: Abu Dhabi Publishers. and Wishart London.

Bible Society of Kenya (1958), *Good News Bible*. Nairobi: Neema Publishers Ltd.

De Beuvoir, S. (1949). *The Second Sex*. Chapa ya Picador Classics (1988) London: Pan Books Ltd.

Eagleton, M (1986) *Feminist Literary Criticism*. New York: Longman.

Ellmann.M. (1968), *Thinking about Women*. New York: Harcourt.

Fiinegan, R. (1970), *Oral Literature in Africa*. London: Oxford University Press

Friedman, B. (1963, *The Feminine Mystique*. New York: Dell.

Gachukia, E. (1993). "Empowering the Kenya Woman".Nairobi: National Committee on the Status of Woman." ( Hayajachapishwa).

Gitau, R. Njoroge (2010). "Nafasi ya Mwanamke katika Utenzi wa Fatuma." Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Hamilton, R. (1978*) The Liberation of Women: A study of Partiachy and Capitalism.* London: George Allen and Unwin publisher Ltd.

Hussein, E. (1970), *Michezo ya Kuigiza*. Nairobi: East African Publishing House.

Hussein, E.N. (1971), *Wakati Ukuta*. Nairobi: Oxford University press.

Jaquette J .S. (1974), *Women in Politics*. NewYork: John Willey and Sons.

Kabira, W. na Nzioki, E. (1993), *Celebrating Women's Resistance*. Nairobi: African Woman's Perspectives.

Kamunde M.E (1983), "Kilio Cha Wanyonge katika Riwaya za Saidi Ahmed Mohammed".Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu Cha Nairobi (Hakijachapishwa)

Kathleen, N. (1979), The *Sisterhood of Man: The Impact of Womens' Changing Roles on Social and Economic Life Around the World*. New York: W.W. Norton, Publishers .

Katola, E (2006), "Udhalimu Dhidi ya Wahusika wa Kike katika Tamthilia za Kiswahili.''Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu Cha Nairobi.

Kiango S. (1997)."Taswira ya Mwanamke katika Tamthilia za Kiswahili za Kenya". Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

Kijumwa, M. (1973), *Utenzi wa Fumo Lyongo*. Dar-es-Salaam: Chuo Kikuu cha Uchunguzi wa Lugha ya Kiswahili.

Kithaka wa Mberia (1997*) Natala*.Nairobi: Marimba Publications Ltd.

Lugano, R.S (1989) "Mwanamke Katika Riwaya za Kezilahabi." Tasnifu ya M.A Chuo Kikuuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Mazrui,A.(1981*), Kilio cha Haki* . Nairobi:Longman Kenya Ltd

Mbatiah M. (2001). *Kamusi ya Fasihi na Nadharia*. Nairobi: Standard Text Books Graphics and Publishing.

Millet, K (1970) *Sexual Politics*. London: Virago Press.

Mitchel, J. (1966), *Women: The Longest Revolution* Essays *in Feminism, Literature and Psychology* London: Virago press Ltd.

Mohammed, S.A. (1980), *Utengano*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Momanyi, C. (2002). "Swala la Uana katika Fasihi ya Kiswahili". Katika Simala. I. *Utafiti wa Kiswahili. Umoja Press.*

_____(1998), ''Usawiri wa Mwanamke Mwislamu katika Jamii ya Waswahili kama Inavyobainika katika Ushairi wa Kiswahili'' Tasnifu ya PhD; Chuo Kikuu Cha Kenyatta.(Haijachapishwa)

Mugambi P. J. (1982). "Uhakiki wa Maudhui katika Tamthilia za Kenya zilizochapishwa." Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu Cha Nairobi. ( Haijachapishwa)

Muhando, P. (1974), *Heshima Yangu*. Nairobi: East Africa Publishing House .

Mwachofi, A.K (1987), *Mama Ee*. Nairobi: Heineman Kenya Ltd.

Mwendarani, B. (2012), ''Taswira ya Mwanamke Katika Tamthilia za Kiswahili.'' Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu Cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Ndungo, C. (1985), "Wanawake na Mabadiliko ya Kihistoria katika Fasihi ya Kiswahili". Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Nicholas, L.J (1986), *Gender and History*. London: Columbia University Press.

Njau, R. na G. Mulaki (1984), *Kenya Women Heroes and their Mystical Power*. Nairobi; RiskPublishers.

Njogu, K na Chimera, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Njogu K .n.w (2011), *Kamusi ya Karne ya 21*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Nyamberi, H. (1997). "Mwamko wa Mwanamke katika Tamthilia za Penina Muhando". Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

Nyerges, A. (1962*). Woman in Hungary*. Budapest: Unwersity Printing House.

Oskaya,G (1981), *From Captivity to Freedom*: *A Woman's Fight*. Nairobi: .Ankara Publishing Ltd.

Ramazanoglu, C. (1989). *Feminism and the Contradictions of Oppression.*London: Routledge.

Saadawi,E(1980), *The Hidden Face of Eve: Women in the Arab World.* London: Ontal Press Ltd .

Tutle, L. (1986) *Encyclopaedia of Feminism* London, Longman Group Ltd.

Wafula, R.M. na Kimani, N. (2007), *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K.W. (2002), *Uhakiki wa Fasihi: Msingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Pheonix Publishers Ltd.

______________(2003), *Kichocheo Cha Fasihi; Simulizi na Andishi.* Nairobi: Focus Publishers

___________ (2003). *Kamusi ya Fasihi, Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Books.

____________ (2003), *Pango*. Nairobi: Focus Publishers Ltd.

_________ (2008*) Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi.* Nairobi: Vide-Muwa Publishers Ltd.

Warner, A. (1934), *Utendi wa Mwanakupona*. London: United Press

Wolgast, E. (1980). *Equality and the Rights of Women*. London: Unlimited Press

Wollstonecraft, M. (1792). *A Vindication of the Rights of Women*. Harmondworths: Penguin. Black Well Publishers.